





**Wazazi** wasakwa wanafunzi 436 kutoripoti shule kidato cha kwanza

UKURASA 3



**TUCHEL ATOA SABABU LUKAKU BENCHI UEFA**

UKURASA 21


# Nipashe

**Alhamisi Februari 24, 2022** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580866

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




RIPOTI MAALUM

# Bei ya gesi haikamatiki

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akishirikiana na viongozi wa vyama vilivyoshiriki kupigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika kukata utepe kufungua rasmi Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere Kibaha, mkoani Pwani, jana. Wengine ni viongozi mbalimbali wa CCM, akiwamo Rais mstaafu, Jakaya Kikwete (kushoto). **PICHA: IKULU**

## Samia ataja malengo Chuo cha Uongozi

UKURASA 3

## Mahakama yamwachia huru kigogo CHADEMA

UKURASA 2


**MICHEZO** **DEWJI AIONYA SIMBA SC CAF** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA




Mratibu Msaidizi wa Polisi, Jane Dotto kutoka Dawati la Jinsia na Watoto la Wilaya ya Kinondoni, akichangia mada kwenye warsha ya kutoa mrejesho wa awali kuhusu utekelezaji wa mradi wa majaribio ya kukabiliana na ukatili wa kingono katika kata za Makumbusho na Mwananyamala mkoani Dar es Salaam juzi. Mradi huo unatekelezwa na Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC), kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA). **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mahakama yamwachia huru kigogo CHADEMA

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemwondolea mashtaka Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Hashim Issa, aliyekuwa akituhumiwa kwa makosa mawili ikiwamo kumchafua na kumdhalilisha Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro, kwa kumwita gaidi namba moja nchini na fisadi.

Uamuzi wa kuondoa mashtaka na kumwachia huru mshtakiwa huyo ulitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Lomuli Mbuya.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali Mwanaamina Komba Kono, alidai Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, amewasilisha hati akionyesha kwamba hana nia ya kuendelea na shauri hilo.

Mwanaamina aliiomba mahakama ikubali maombi hayo na kumwachia huru mshtakiwa na Hakimu Lomuli alikubali maombi hayo na kumwachia huru mshtakiwa.

Issa ambaye ni Mkazi wa Mbweni, Kiembe Samaki, alipanda kizimbani kwa mara ya kwanza Oktoba 7, mwaka jana.

Alikuwa anakabiliwa na mashtaka mawili anayodaiwa kuyatenda Oktoba Mosi mwaka jana maeneo ya Kinondoni B, Mtaa wa Ufipa.

Inadaiwa katika shtaka la kwanza kwamba Issa alichapisha taarifa za uongo kwa njia ya kompyuta na kusambaza katika mtandao wa YouTube kwa lengo la kumchafua na kumdhalilisha IGP Sirro.

Mshtakiwa anadaiwa kuchapisha kwamba IGP Simon Sirro ni gaidi namba moja nchini Tanzania na fisadi.

Katika shtaka la pili alidaiwa kutenda kosa la uchochezi kwa lengo la kutengeneza chuki na taharuki kwa wananchi wa Tanzania dhidi ya IGP kwa kutoa maneno kwamba Simon Sirro ni gaidi namba moja nchini na fisadi.

Mshtakiwa alikuwa akiwakilishwa na Wakili Alex Masaba na alikuwa nje kwa dhamana ya masharti ya kuwa na wadhamini wawili waliotia saini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni tatu, wawe na barua ya utambulisho, wawe na vitambulisho vya mpigakura au kitambulisho cha taifa.

Baada ya kuachiwa huru na mahakama jana, 'kigogo' huyo wa CHADEMA alipelekwa Kituo Kikuu cha Polisi jijini Dar es Salaam ambako baadaye aliachiwa kwa dhamana na haijajulikana kama atashtakiwa tena au la.

### RIPOTI MAALUM

# Bei ya gesi sasa haikamatiki

**Na Jenifer Gilla**

"NIMEONA nitumie mkaa kwa sasa mpaka bei ya gesi itakaposhuka, maisha ni magumu. Gesi ya kilo 15 ninayoinunua kwa Sh. 25,000, ninatumia kwa mwezi na wiki moja wakati gunia la mkaa la 27,000 ninalitumia kwa miezi miwili," Tina Shemweta, mkazi wa Ubungo mkoani Dar es Salaam anawasilisha kilio chake.

Tina (32), mama wa mtoto mmoja, analalamika kuwa kwa sasa amelazimika kuachana na matumizi ya gesi ya kupikia (LPG) kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo kutoka Sh. 20,000 miezi minne iliyopita hadi Sh. 25,000 kwa mtungi mdogo wa ORYX.

Anasema amelazimika kurejea kwenye matumizi ya mkaa kwa kuwa familia yake haiwezi kumudu bei mpya za gesi.

Jamila Mwinchea, mkazi wa Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam, ana kilio kama cha mtangulizi wake Tina, akilalamika kuwa sasa ananunua gesi ya kupikia kwa Sh. 58,000 kutoka Sh. 45,000 miezi minne iliyopita kwa mtungi wa Kg 30 wa kampuni ya ORYX.

"Gesi imepanda sana dada yangu (mwandishi), si mchezo. Kuna ongezeko la Sh. 13,000 kwa kipindi cha miezi minne tu, na inavyoonekana serikali isipoingilia kati itazidi kupaa," anatahadharisha.

Alphonce George, mkazi wa Kimara Baruti wilayani Ubungo, anasema bei ya mtungi wa Kg 30 wa kampuni ya gesi ya Taifa kwa sasa kwenye maeneo yao imefikia Sh. 53,000 kutoka Sh. 45,000 ilivyouzwa awali.

"Yaani wanapandisha halafu wanasikilizia, watu wanalalamika wakiona wameacha wanapandisha tena. Yaani tumetoka kununua kwa Sh. 45,000 mpaka Sh. 53,000 sasa. Tunaiomba serikali iingilie kati kutunusuru, hali ya maisha ni ngumu," analalama.

Jana mchana, Nipashe ilipita kwenye maduka yanayouza nishati hiyo maeneo ya Mwenge wilayani Kinondoni na kukuta mtungi wa Kg 15 wa gesi ya ORYX unabadilishwa kwa Sh. 24,000 na Kg 30 Sh. 58,000 wakati gesi ya Taifa Kg 15 unabadilishwa kwa Sh. 22,000 na Kg 30 Sh. 54,000.

Rose James ni muuzaji wa gesi Tabata jijini Dar es Salaam. Anasema wanalazimika kupandisha bei ya bidhaa hiyo kwa madai kuwa imepanda wanakoinunua kwa wauzaji wa jumla.

"Unafikiri tunapenda kuuza hii bei dada yangu? Na sisi wale wanaotuletea kwa jumla wametupandishia. Kwa mfano, gesi ya ORYX mtungi wa kilo 15 tunauziwa 20,000 na wa kilo 30 tunauzwa Sh. 53,000 wakati gesi ya Taifa mtungi wa kilo 15 tunauziwa Sh. 17,000 na kilo 30 Sh. 58,000," anafafanua.

**HALI ILIVYO KITAIFA**

Kwenye maduka ya gesi yaliyoko Kwa Mrombo, Kata ya Muriet Wilaya ya Arusha, Nipashe ilimshuhudia Febronia James akinunua gesi ya Manjis kwa Sh. 54,000 kwa mtungi mkubwa huku udadisi ukibaini mtungi mdogo ulikuwa unauzwa kwa Sh. 21,500.

Mjini Njombe Nipashe ilishuhudia jana majira ya saa nane mchana mtungi kubwa wa kampuni ya ORYX ukibadilishwa kwa Sh. 55,000 huku baadhi ya maduka wakibadilisha kwa Sh. 58,000 wakati mtungi mdogo ukibadilishwa kwa Sh. 24,000.

"Kweli bei ya gesi imepanda ghafla, yaani imepandishwa kutoka Sh. 52,000 hadi Sh. 58,000, hii ni mbaya kwa kweli," alilalamika Aghata Kiyeyeu, mkazi wa mjini Njombe.

"Kwanza tuliamini gesi ndio mbadala wa mkaa lakini hali ni tofauti. Kupanda panda huku kwa bei ya gesi ni hatari kwa mazingira yetu kwa sababu watu watarudi kwenye mkaa tu," anaonya.

Mjini Moshi jana, mfanyabiashara Mwanajuma Hassan mwenye duka la gesi ya kupikia katika Mtaa wa Uswalini, aliiambia Nipashe mtungi mdogo wa gesi anauza kwa bei ya jumla Sh. 48,000 na kujaza ni Sh. 22,000.

"Mtungi mkubwa bei ya kuuza ni Sh. 94,000 na kujaza ni Sh. 55,000 kwa Kampuni ya ORYX. Taifa na Orange, mdogo bei ya kuuza ni Sh. 39,000 na kujaza ni Sh. 20,000. Gesi ya Taifa bei ya kuuza ni Sh. 42,000 na kujaza ni Sh. 20,500.

Mjini Mwanza, Nipashe ilishuhudia jana majira ya saa 10 jioni mtungi mdogo wa kampuni ya ORYX ukibadilishwa kwa Sh. 24,000 na mkubwa Sh. 56,000 huku gesi ya Taifa ikibadilishwa kwa Sh. 22,000 kwa mtungi mdogo na Sh. 54,000 kwa mtungi mkubwa.

Jijini Dodoma, bei ya kujaza mtungi wa gesi aina ya ORXY ilikuwa Sh. 24,000 kwa mtungio mdogo kwenye maduka ya Mtaa wa Mtendeni huku mtungi mkubwa ukibadilishwa kwa Sh. 55,000 huku ile ya gesi ya Taifa ikibadilishwa kwa Sh. 22,500 na Sh. 53,000, mtawalia.

Miezi saba iliyopita serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitoa zuio la kupandisha kiholela bei ya gesi ya kupikia.

Julai 17, mwaka jana, EWURA ilitangaza zuio hilo mpaka pale itakapopokea na kupitia mapendekezo ya hoja za uhalali wa kupandisha bei ya hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Edward Chibulunje, aliziagiza kampuni za gesi kuwasilisha EWURA maelezo ya uhalali wa kupandisha bei hizo kwa ajili ya uhakiki, huku akionya kampuni itakayoshindwa kufuata agizo la udhibiti kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

***Taarifa za ziada na Cynthia Mwilolezi, Tumaini Mafie (ARUSHA), Mary Mosha (MOSHI), Ibrahim Joseph, Renatha Msungu (DODOMA), Elizabeth John (NJOMBE), Richard Makore (MWANZA) na Maulid Mmbaga (DAR).**

HABARI KITAIFA

## AAFP yageukia hamasa chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Alliance for African Farmers Party (AAFP), kimejitosa katika kampeni ya kuhamasisha Watanzania kujitokeza kupata chanjo ya UVUKO-19 ili kulinda afya zao.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Nancy Mrikaria, alisema hayo jijini Dar es Salaam jana, alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kufafanua kuwa karibu viongozi wote wa AAFP wameshachanjwa.

"Tumewaelekeza viongozi wa chama kote nchini, kila wanapokutana katika vikao vya kawaida, wagusie chanjo na hata wanapokuwa katika shughuli zao za kawaida mitaani, waelezee umuhimu wa chanjo," alisema Mrikaria.

Kiongozi huyo alisema wanatumia njia hiyo kuhamasisha chanjo, kwa kuwa chama chao hakina fungu la fedha la kuzunguka nchi nzima na kuitisha mikutano ya kuhamasisha watu kuchanja.

"Tunatamani kuzunguka nchi nzima kuhamasisha chanjo, lakini hatuna uwezo wa kifedha, hivyo tumeona tuhamasishe kwa njia hii tunayoitumia sasa ikiwamo ya vikao vyetu au tunapoitwa katika vyombo vya habari kujadili jambo fulani, tunachomekea suala la chanjo ya corona," alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema chama chao kinaunga mkono juhudi zote zinazofanywa na serikali kwenye suala la chanjo ya UVIKO-19, na kwamba viongozi wote kuanzia ngazi ya chini hadi taifa wamechanjwa.

"Chama chetu kimeona kishiriki mpango shirikishi na harakishi awamu ya pili wa mapambano dhidi ya UVIKO-19, ambao unaelekezwa na serikali ili kutoa mchango wetu kwenye kampeni muhimu ya chanjo," alisema.

Mrikaria alisema, chama chao kinaamini kuwa kampeni ya chanjo ya ugonjwa huo ni shirikishi vikiwamo vyama vya siasa, viongozi wa dini, wa mitaa, taasisi za binafsi na hata wanahabari na wengine.

"Makundi yenye ushawishi katika jamii vikiwamo vyama vya siasa, yanatakiwa kushiriki kampeni ya chanjo, ingawa kuchanja ni hiari, lakini inawezekana wengine hawajachanja kutokana na upotoshaji," alisema.

Alisema, uhamasishaji huo ambao una utoaji wa elimu sahihi kuhusu chanjo, unaweza kusaidia watu wengi kujitokeza kupata huduma hiyo ambayo inatolewa bure katika vituo vilivyoko maeneo mbalimbali nchini.

"Nitoe ombi kwa serikali kuangalia uwezekano wa kuvipa fungu la fedha vyama ambavyo havina ruzuku kama chetu, ili tushiriki kikamilifu katika kampeni hizi za kuhamasisha wapigakura kupata chanjo," alisema.

# Rais Samia ataja malengo ya Chuo cha Uongozi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuanzishwa kwa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere ni hatua mojawapo ya kuwaandaa vijana kubadilisha mitazamo na mawazo ya viongozi wa zamani katika kuisaidia nchi.

Samia aliyasema hayo jana wakati akizindua shule hiyo ya Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere kilichoko Kwamfipa Kibaha ambacho kimejengwa kwa ushirikiano wa vyama sita vya ukombozi Kusini mwa Afrika.

Rais Samia alisema kuanzishwa kwa chuo hicho ni kujibu changamoto na kuimarisha vyama katika utendaji wao kwani mafunzo yatakayokuwa yanatolewa yatahusu uongozi na itikadi masuala ambayo yanazikabili nchi nyingi.

Alisema uwapo wa chuo hicho na kuwaweka pamoja vijana ambao wanafanya kazi kwenye vyama na serikali za nchi hizo itawabadilisha na kwenda mahali ambako serikali inataka

Aliwapongeza viongozi watangulizi akiwamo Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, ambaye alishirikiana na viongozi wa nchi nyingine kukubaliana wazo la kujenga chuo hicho cha uongozi.

Rais alitoa wito kwa chuo hicho kufanya kazi iliyokusudiwa ya kubadilisha maono ya vijana wa nchi za Afrika.

"Wananchi wetu wana imani ya kuongozwa na vyama vyetu tawala miaka mingi ijayo hivyo tumeamua kuonyesha njia kwa kuja na chuo hiki kitakachotoa mafunzo kwa watu wetu," alisema.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema ujenzi wa chuo hicho ni makubaliano ya vyama rafiki vya ukombozi vya Afrika mwaka 2012 huko Harare, Zimbabwe.

Chongolo alishukuru mchango wa Jamhuri ya Watu wa China kwa kukubali kugharamia ujenzi wa chuo hicho.

Alisema chuo hicho kitaanza kuchukua wanafunzi Machi mwaka huu na kwamba kila chama kitaleta makada wake kuanza mafunzo ya awali.

Chongolo alisema kuwa mafunzo yatakayokuwa yanatolewa katika chuo hicho ni ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu na yataendana na mahitaji ya ndani na nje kukabiliana na mabadiliko ya kisiasa.

"Tuna uhakika uwekezaji huu utaleta uhusiano mazuri kiuchumi kwenye hizi nchi za Afrika na shule hii ya kihistoria tunalenga kujenga mahusiano mazuri na vyama vya nchi vyenye mlengo mmoja.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi wa chuo hicho, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM anayehusika na Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali (mstaafu) Ngemela Lubinga, alisema hadi kukamilika shule hiyo imegharimu Sh. bilioni 105.7.

Alisema chuo hicho kimejengwa kwa makubaliano ya nchi sita ambazo vyama vyake vilishiriki kwenye ukombozi wa Afrika na kwamba jiwe la msingi liliwekwa na Hayati Rais John Magufuli Julai, 2018 na kilitarajiwa kukamilika mwaka 2020.

Lubinga alisema muda wa kukamilika kwa chuo hicho ulichelewa kutokana na vifaa kushindwa kufika kwa wakati kwa sababu ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema chuo hicho ambacho eneo lake lina ukubwa wa ekari 22 ni ekari 10.1 pekee ambazo zimetumika na kimekamilika kwa asilimia 100 huku kikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kwa wakati mmoja.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipata maelezo ya uendeshaji wa shughuli za kampuni ya madini ya Barrick kwa Meneja wa kampuni hiyo nchini, Georgia Mutagahywa (kushoto), wakati alipotembelea maonyesho kwenye mkutano wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania 2020, jijini Dar es Salaam juzi. Barrick ni mdhamini mkuu wa mkutano huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi wasakwa watoto 436 kutoripoti kidato cha kwanza

**NA ABDALLAH KHAMIS,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amewaagiza watendaji wa ngazi ya vijiji na kata katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba kufanya msako wa nyumba kwa nyumba na kuwakamata wazazi wa watoto 436, walioshindwa kuripoti shuleni kuanza kidato cha kwanza kwa mwaka 2022.

Gaguti alitoa agizo hilo baada ya kupewa taarifa kuwa wanafunzi hao wameshindwa kusajiliwa kwa ajili ya kuanza masomo, baada ya kuchaguliwa kujiunga na shule za sekondari kutokana na matokea yao ya darasa la saba mwaka 2021.

Amesema msako wa kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wazazi wa watoto wasiofika shule uwe endelevu katika halmashauri hiyo kwa lengo la kuwafanya wazazi wawajibike kuhakikisha watoto wao wanapenda shule.

Brigedia Jenerali Gaguti alitoa agizo hilo katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, alipofanya kikao na wadau wa elimu wakati wa ziara ya kufuatilia utekelezaji wa mpango wa elimu katika mkoa huo, uliolenga kuangalia na kujadili mpango wa halmashauri moja moja na utekelezaji wake.

Alisema ni aibu kila wakati kwa mkoa wa Mtwara kuwa sehemu ya mikoa inayofanya vibaya katika matokeo yake ya mitihani mbalimbali kwa sababu ya baadhi ya wadau kutokutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Aliwaonya watendaji na wadau wa elimu kutotafuta sababu wanapokuwa na vikwazo, badala yake wajikite kuvitatua kwa kuangalia namna nzuri ya kushirikisha jamii.

"Kwenye sekta ya elimu walimu wamelalamika, hapa mkurugenzi ameeleza kuwa wanafunzi 436 hawajaripoti, ninyi mpo, ninawaelekeza kwa kushirikiana na walimu na viongozi wengine nendeni nyumba hadi nyumba chomoa baba, chomoa mama, chomoa mlezi ambaye ameridhia mtoto asiende shule, fanyeni hivi mpaka watakapopenda shule," alisema Gaguti.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nanyamba, Thomas Mwailafu, alimweleza Gaguti kuwa katika udahili wa wanafunzi, waliopaswa kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, halmashauri hiyo imefikisha asilimia 81 ya wanafunzi wote huku asilimia 19 wakiwa hawajaripoti.

Mwailafu alisema hali hiyo ya watoto kutoripoti shuleni inachangiwa kwa kiasi kikubwa na wazazi na walezi kutokuthamini masomo, hali inayotishia mustakabali wa Taifa kwa miaka ijayo.

Ofisa Elimu Mkoa, Kiduma Mageni, alisema idadi ya wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza katika halmashauri hiyo ni tofauti na idadi ya wanaomaliza kidato cha nne, kutokana na baadhi kuacha shule wanapofika kidato cha pili.

"Kuna sababu zinazochangia idadi ya wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza kuwa tofauti na wanaomaliza, lakini kubwa ni umbali wa baadhi ya maeneo, wazazi kuwashawishi watoto wao wasifanye vizuri katika mitihani ya kidato cha pili pamoja na baadhi ya shule kushindwa kukidhi mahitaji ya chakula cha mchana kwa wanafunzi," alisema.

# Majaliwa aiagiza wizara udhibiti utoroshaji madini

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Madini kuhakikisha inasimamia ipasavyo sekta ya madini nchini na kudhibiti utoroshaji wa madini katika maeneo mbalimbali.

Majaliwa alitoa maelekezo hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifunga mkutano wa nne wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini na kuagiza mambo matano kwa wizara tatu.

Akizungumza katika mkutano huo, aliitaka Wizara ya Madini kuendelea kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini na udhibiti wa utoroshaji wake.

"Watu wa madini, serikali, vyombo vya ulinzi na usalama lazima msimamie hili tunataka tujue ni kiwango gani cha madini kinachopatikana, tunaingiza pato la mtu mmoja mmoja kiasi gani, halmashauri gani zinachimba madini na kiasi gani," alisema.

Agizo lingine aliitaka wizara hiyo isimamie na kuratibu maazimio ya mkutano huo ili taarifa za utekelezaji ziwasilishwe katika mkutano utakaofanyika mwakani.

"Wizara ya Fedha (Mipango) mwendelee kuimarisha mifumo ya mawasiliano na watu hawa wa madini ili waweze kutoa kero zao, mrejesho wa mafanikio yao kwa wizara husika na nyie mnapokutana na matatizo mnapata nafasi ya kuzishughulikia, tutengenezeni mfumo wa ushirikishwaji," alisema.

Majaliwa alitaja jambo la nne ni Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ihakikishe inatambua maeneo yote rasmi kwa ajili ya shughuli za madini na viwanda.

"Masoko ya madini na viwanda yatambuliwe, tusiache hili kwa Wizara ya Madini peke yake, TAMISEMI mshiriki kikamilifu kwenye uratibu wa hili ili TAMISEMI na Wizara ya Madini muwe mnazungumza lugha moja, wakuu wa mikoa nyie ndiyo wasimamizi wakuu wa shughuli za serikali kule kwenye mamlaka zenu haya maagizo yafanyike kwenye halmashauri zenu, pamoja na wakuu wa wilaya," aliagiza.

Jambo la tano aliitaka Wizara ya Madini iendelee kuvinadi nje ya nchi viwanda vilivyoko ili kuvutia wadau wengine kuja kuwekeza.

Majaliwa alitumia mkutano huo kuwataka wawekezaji wakubwa katika sekta hiyo wasaidie wengine wayajue masoko ya madini yaliyoko.

Alisema serikali imeanzisha masoko ya madini kuanzia ngazi ya wilaya na mikoa ili kuyaunganisha yale ya awali, kati na makubwa.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wafanyabiashara wa madini nje ya mipaka ya Tanzania kulitumia soko la hapa kwa kuyaleta madini yao.

Majaliwa alisema suala la uongezaji thamani madini limekuwa likipigiwa kelele muda mrefu na kuwataka wawekezaji wapanue wigo kwa kununua mitambo ya kufanya shughuli hiyo.

"Tunataka wawekezaji wengi wa kuongeza thamani waje Tanzania, Tanzanite ilikuwa inaonyesha inazalishwa Ulaya kitu ambacho siyo sahihi, tunataka wale waliokuwa wanakwenda huko watue KIA, mkiongeza thamani mtapata faida za kutosha.

Pia aliwataka wawekeze kwenye uchenjuaji madini ili wapate madini kwa asilimia 99.

Kadhalika alikitaka Chama cha Wachimbaji Wadogo kuendelea kulisimamia kundi hilo ili liweze kuingia kwenye uwekezaji mkubwa.

Aidha, alisema nchi ina masoko 44 na vituo 70 vya kuuzia madini.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko alisema wizara itakaa ili kushughulikia suala la wachimba madini ya chumvi kwa kuzungumza nao na kuona kama uzalishaji wao unatosheleza mahitaji ya ndani na kama hautoshelezi wataangalia namna ya kuwawezesha kuchimba ya chumvi ya kutosha ili kuepuka kuagiza madini hayo nje ya nchi.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu, Dk. Zainabu Chaula (kulia), akizungumza na maofisa wa Benki ya NMB, alipokutana nao kwenye mkutano wa viongozi wa wamachinga, jijini Dodoma jana. NMB ni mfadhili mkuu wa mkutano huo, ulioshirikisha viongozi hao kutoka mikoa yote nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakulima, vijana kuneemeka bil. 400/- kilimo

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imetenga zaidi ya Sh. bilioni 400 kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wakulima kujiimarisha katika kilimo cha biashara.

Fedha hizo zitatolewa kwenye vikundi maalum baada ya mchakato wa kuwapatia elimu ya masuala ya kilimo kukamilika kupitia wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

Akizungumza na waandishi jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema kuanzia sasa vijana wanapaswa kukaa mkao wa kula kwamba mikopo hiyo itatolewa kwa riba ya asilimia tisa.

Nyabundege alisema alisema Desemba, mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan aliitapatia TADB mtaji wa Sh. bilioni 208 kutoka mtaji wa Sh. bilioni 60 uliokuwapo awali.

"Ni mtaji mkubwa ambao haujawahi kutolewa hapa nchini. Baada ya kupewa mtaji huo tuliingia kwenye orodha ya benki 10 zenye mtaji mkubwa nchini. Mtaji huu utawafikia zaidi ya Watanzania asilimia 65," alisema.

Nyabundege alisema Februari 12, mwaka huu, Rais Samia akiwa ziarani Ufaransa aliingia mkataba wa masharti nafuu na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (FAD) wa Euro milioni moja (Sh. bilioni 2.6) kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakulima na kuimarisha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Alisema Rais Samia pia aliingia mkataba wa masharti nafuu na FAD wa Euro milioni 80 (Sh.bilioni 210) zitakazotumika kusaidia uendelezaji wa sekta ya kilimo nchini.

Pia alisema serikali imekuwa katika mazungumzo na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kwa ajili ya kusaidia sekta ya kilimo nchini, kwamba shirika hilo limekubali kutoa Dola za Marekani milioni 40 (Sh. bilioni 92).

Kadhalika, Nyabundege alisema Taasisi ya Bill & Melinda Gates nayo imetoa msaada wa Dola za Marekani milioni saba (Sh. bilioni 16.2) kwa ajili ya kusaidia sekta ya kuchakata maziwa.

"Tunajivunia kuwa na Rais ambaye ndani ya mwaka mmoja ametuletea zaidi ya Sh. bilioni 400. Hii ni namna gani anaonekana anawajali Watanzania ambao asilimia kubwa wamewekeza kwenye sekta ya kilimo," alisema.

Aliongeza kuwa zaidi ya Watanzania 22,500 watanufaika kupitia fedha hizo, kwamba kwa sasa sehemu ya fedha hizo zimeanza kutolewa.

Aidha, Nyabundege alisema TADB iko katika mkakati wa kununua mitamba 1,750 kwa ajili ya kuwapatia wakulima ili waweze kujikwamua kupitia sekta ya maziwa.

# Mafunzo yakwamisha kesi ya kina Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imeahirisha kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita kwa kuwa mawakili wa Jamhuri wanaosikiliza shauri hilo wako katika mafunzo ya kuongeza weledi.

Mbali na Sabaya washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanaokabiliwa na mashtaka matano yakiwamo ya matumizi mabaya ya madaraka, kuongoza genge la uhalifu, kujihusisha na vitendo vya ruswa na utakatishaji wa fedha.

Akizungumza mahakamani huko jana, Wakili wa Serikali, Neema Mbwana, aliiomba mahakama kuahirisha kusikiliza shauri hilo kwa kuwa jopo la mawakili wanaosimamia kesi hiyo lipo kwenye mafunzo ya kuwaongeza weledi.

"Mheshimiwa hakimu, tunaomba mahakama yako tukufu kuahirisha usikilizwaji wa shauri hili kwa kuwa jopo la mawakili wanaosimamia kesi hii wapo kwenye mafunzo ya kuwaongezea weledi," alidai Neema.

Wakili wa Upande wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai walikuwa tayari kuendelea na usikilizaji wa kesi lakini kwa kuwa upande wa mashtaka wametoa ombi la kuahirishwa, hawakuwa na pingamizi.

"Ombi letu tunaomba tarehe itakayopangwa kwa ajili ya kesi kuendelea iwe ya karibu ili kufikia tamati mapema iwezekanavyo," alidai Mahuna.

Baada ya kusikiliza maombi hayo, Hakimu Patricia Kisinda aliahirisha shauri hilo hadi Machi 7, mwaka huu, itakapoendelea mahakamani huko.

"Mahakama imekubali ombi la wakili wa Jamhuri, hivyo tunaahirisha usikilizwaji wa kesi hii hadi Machi 7, mwaka huu, majira ya saa 3:00 asubuhi," alisema Hakimu Kisinda.

Hadi sasa mashahidi watatu wa utetezi wameshapanda kizimbani kutoa ushahidi wao ambao ni mke wa mshtakiwa wa kwanza, Jesca Thomas, Ole Sabaya na Silvester Nyegu.

Katika kesi hiyo mashtaka ni kuongoza genge la uhalifu; kujihusisha na vitendo vya rushwa; kujihusisha na vitendo vya rushwa; matumizi mabaya ya madaraka (yanayomkabili Ole Sabaya peke yake); na utakatishaji wa fedha linalowakabili washtakiwa wote saba.

# TANGAZO

Summonsto an Accused Person (S.91)

Crime Form No. 6 (Approvedby the High Court under S: 352 of Cr. P.C)

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE RESIDENTMAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO. 377 OF 2020**

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**EDES APOLINARY MSALE**……………………………………………………**ACCUSED PERSON**

**TO:**

**EDES APOLINARY MSALE**
**PLOT NO. KND/UNUNG/UK32/32**
**KISIWANI AREA, UBUNGO**
**UBUNGO MUNICIPALITY**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge of **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED** in the name of the Republic to appear in thisCourt on the …31…day of…MARCH….., 2022 at 08:00a.m., or soon thereafter as the case can be heard.

**Herein fail not.**

**GIVEN** under my hand the **SEAL** of the Court this…17…day of…FEB…, 2022.

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

**RECEIVED BY:**
**NAME**……………………………………………………
**RELATIONSHIP, IF ANY**……………………………………
**DATE**……………………………………………………

**SIGNATURE**……………………………………………………

216720002

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF GEITA**
***(AT GEITA)***

**CRIMINAL CASE NO. 01 OF 2022**

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**ELEMECH ENGINEERING (TANZANIA) LTD**…………………………**ACCUSED PERSON**

**To:**
Managing Director
Elemech Engineering Limited
Sinza Area, Shekilango Road
Off the Makaburini Traffic Lights
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge on **TRADING AND/OR CARRYING ON BUSINESS AS A CONTRACTOR WHILE NOT REGISTERED CONTRARY TO SECTION 22(1)(D) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the…22nd…… day of……MARCH………… 2022 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this …14th day of FEBRUARY……… **2022**

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE GEITA.

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship

Date……………………………………

216720002

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO. 203 OF 2021**

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**OILCOM (T) LTD**…………………………………………………**ACCUSED PERSON**

**To:**
Chief Executive Officer
Oilcom (T) Limited
Plots Nos. 4 & 312, Mandela Road,
Kurasini Area, Ilala Municipality, Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the….01…. day of ………03………… 2022…. at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ……26… day of ………01……………2022…..

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship
Date……………………………………

216720002

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
***(AT KINONDONI)***

**CRIMINAL CASE NO. 20[illegible] OF 2021**

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**OILCOM (T) LTD**…………………………………………………**ACCUSED PERSON**

**To:**
Chief Executive Officer
Oilcom (T) Limited
Plots Nos. 4 & 312, Mandela Road,
Kurasini Area, Ilala Municipality, Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the….01…. day of ………03………… 2022…. at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this …26… day of ………01……………2022….

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………………

Signature………………………………

Qualification/Relationship
Date……………………………………

216720002

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakulima wapewe elimu kukabili viwavijeshi, nzige

**HIVI** karibuni timu ya watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), ilitembelea Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro kujionea uharibifu katika hekari 4,976 za mpunga na 228 za mahindi zilizoharibiwa na wadudu aina ya viwavijeshi.

Wataalamu hao walikwenda pia kuwafundisha wakulima namna ya kukabiliana na wadudu hao hasa kwenye matumizi sahihi ya viuatilifu.

Pia wanatakiwa kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo kwa kuwa kuna viuatilifu vinavyoua viwavijeshi, ndiyo maana wanashauri kufuata utaalamu ili kufanikiwa.

Baadhi ya wakulima walisema kuna wenzao wameenda kununua dawa bila kufuata ushauri, walipopulizia waliendelea kuwapo, jambo ambalo ni hasara kwao.

Wakulima hao walieleza kuwa kwa zaidi ya miaka 70 ni mara ya kwanza wanaona viwavijeshi vikishambulia mpunga kwa kasi ya ajabu, jambo ambalo linahitaji msaada wa kipekee.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, alieleza viwavijeshi wako kwenye kata 12 kati yake saba zimeathirika zaidi, na kwamba serikali imepeleka lita 90 za viuatilifu vya kuwagawia wakulima.

Aidha, alisema wanawasiliana na Wizara ya Kilimo ili kupata lita 1,500 za kupeleka maeneo mengi zaidi kuwasaidia wakulima kukabiliana na wadudu hao waharibifu.

Kuwapo kwa wadudu hawa ni dalili mbaya kwa usalama wa chakula kwa ujumla, ikiwa bado wakulima wa mikoa ya kaskazini hawajasahau maumivu yaliyoachwa na nzige ambao walianzia Ethiopia na kusambaa Kenya hadi Tanzania.

Ni muhimu serikali kwa kutumia wataalamu wake kupeleka elimu sahihi kwa wakulima, ili wanapoona dalili wajue ni dawa gani sahihi kwa wadudu hao, katika kuepuka uharibifu.

Tunatambua uwapo wa maofisa ugani kwenye ngazi za kata ambao moja ya jukumu lao ni kusaidia wakulima, wanatakiwa kuhakikisha katika mpango kazi wao kuwa wamewafikia na kuwapa elimu stahiki. Kilimo ni uti wa mgongo ni muhimu kukipa uzito unaostahili kwa kuhakikisha wazalishaji wana taarifa sahihi ili wafanye maamuzi sahihi, tunaamini wakulima hawa wasingepoteza fedha kwa kununua dawa ambazo hazijaua wadudu kama wangekuwa wamepata taarifa sahihi.

Tuna vyuo vya kilimo ambavyo vinafundisha wataalamu ambao wanaajiriwa serikalini na kwenye sekta mbalimbali nchini, ipo haja kuwatumia kwa manufaa ya wazalishaji nchini.

Pia, ipo haja serikali kufuatilia kwa kina madai ya kuwapo kwa viuatilifu visivyo na ubora ambavyo wakulima wameingia hasara wakanunua, kuacha hivyo ni hasara kwao na nchi kwa ujumla kwa kuwa hawatazalisha na kiasi cha chakula tarajiwa kitapungua.

Baadhi ya wabunge mara kadhaa wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge walipaza sauti wakitaka kauli ya serikali juu ya kuwapo kwa viuatilifu hivyo ambavyo ni hatari.

Lazima mamlaka zifanye kazi kwa kushirikiana kukabili uingizwaji sokoni wa bidhaa hizo ambazo ni hatari kwa maisha ya watu na hasara kubwa.

Pia serikali iharakishe kufikisha viauatilifu sahihi kwa wakulima ili kuepusha madhara zaidi, hasa kusambaa kwa wadudu hao kuepusha njaa inayoweza kutokea na kuleta athari.

Serikali ije na mkakati kuwafikia wakulima hasa kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo, ili iwe rahisi kukabiliana na wadudu waharibifu kwenye mazao na kupata pembejeo nyingine muhimu.

Bado kuna nafasi ya kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na kilimo kuwafikia waliko, lakini kuhakikisha hali ya udongo, uchaguzi sahihi wa mbegu na dawa za kutumia, ili kuzalisha kwa wingi hasa wakati huu ambao kuna changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha vipindi vya mvua kubadilikabadilika.

Lakini, lengo la kuwa na vyuo vya kati na vikuu vya kilimo kama Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), ni kupika wataalamu ambao watakuwa msaada wa nchi, ambao unapaswa kuonekana kupitia wakulima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Salome Mwasamale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mbinu kufaulu sekondari, tukajifunze kwao wakuu Mwakyambiki, Orenda

**NIDHAMU** ni kitu muhimu sana katika maisha. Nimegundua kuwa na nidhamu kunafungua njia ya mafanikio kila mahali, iwe kazini unaweza kujikuta unaangukia nafasi ya mfanyakazi bora, pia kwenye familia utakuwa mtoto mpendwa, kwenye ndoa utapendwa sana na mwenza, hadi wakwe.

Mara zote, nidhamu imebaki kuwa sehemu ya mkakati unaotumiwa na shule nyingi kuhakikisha mafanikio yao na kuongeza ufaulu wa watoto wao wa kike na kiume.

Hivi sasa katika baadhi ya shule binafsi, kujiunga nazo kuna sharti huwa wanalitanguliza, mbali na uwezi kitaaluma, pia wanadai nidhamu. Maana yake nini? Inaangukia maana mtu anapokuwa na uelewa mkubwa, lakini nidhamu duni, nafasi hiyo inapotea.

Pia imegundua baadhi ya shule za serikali zimedumisha nidhamu na zinafanya maajabu makubwa katika matokeo yote iwe kidato cha pili, nne au cha sita.

Nidhamu ikisimamiwa vizuri katika shule zetu za serikali tutashuhudia mapinduzi makubwa ya kielimu, huku tukiboresha miundombinu kuongeza vyumba vya madarasa na madawati, hali itakuwa nzuri sana.

Hongera serikali inayoongozwa na Mama Samia Hassan Suluhu, kupeleka fedha nyingi iwezekanavyo za UVIKO-19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na madawati yake (full package), sasa walimu, wazazi na wanafunzi boresheni nidhamu shuleni mpate matokeo mazuri.

Juma Orenda, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mbondole, iliyopo katika kata ya Msongola jijini Dar es Salaam, alituthibitishia hilo kwa vitendo. Nidhamu ni moja ya nguzo katika ufaulu.

Orenda alituambia Shule ya Sekondari Mbondole kwa takribani miaka mitano mfululizo, ilishindwa kufanya vizuri huku ikiambulia kushika mkia katika matokeo yake ya kidato cha nne, lakini tatizo likagundulika ni nidhamu.

"Ufaulu wa mwanafunzi unaenda sambamba na kuwa na nidhamu bora na 'usmati' wa kimwili na kiakili. Nidhamu mbovu haiwezi kuleta matokeo mazuri hata siku moja," akatamka.

Niliwahi pia kudadadisi katika Shule ya Sekondari Nguvu Mpya katika Kata ya Chanika jijini Dar es Salaam, nayo kwa takribani miaka 10 haijawahi kuonja daraja la kwanza kutokana na dai la nidhamu duni, mbovu iliyokuwapo shuleni hapo badala yake ikiambulia kushika nafasi za mwisho kabisa kitaifa.

Nipashe ilikutana na Mkuu wa Mkuu mpya wa shule hiyo, Daniel Mwakyambiki, aliyeletwa kutoka katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Jangwani, ambako alikuwa Mwalimu wa Nidhamu. Naye akaangukia hoja nidhamu, ni kipaumbele chake ili kuiinua shule hiyo kitaaluma.

Miezi saba baada ya kuripoti shuleni hapo na kuboresha nidhamu. Mwalimu Mwakyambiki, alifanikisha kupata daraja la kwanza na kuinua upya matumaini ya wananchi yaliyopotezwa kabisa na shule hiyo.

"Ufaulu kwa watoto wetu wa shule za serikali au kata unawezekana cha msingi tuongeze bidii tudumishe nidhamu, tusiwakatie tamaa watoto wetu," alisema.

Unaweza kujiuliza kwanini wanafurahia ufaulu huo wa watoto wachache? Lakini wao wanajua maumivu waliyoyapata katika kukosa kabisa, hivyo uchache huo unawapa matumaini makubwa kwa wengi.

Sasa wazazi, walimu, wanafunzi na viongozi mbalimbali wa kata wanapambana katika kuhakikisha nidhamu haishuki na shule hizo mwaka huu ufaulu unaongezeka.

Hongereni walimu Orenda na Mwakyambiki kwa jitihada zenu hizo msibweteke sasa, pambaneni kudumisha nidhamu na kuongeza ufaulu. Mimi itakuwa mmoja wao wa kufuatilia mwenendo wa shule zenu.

Wakuu wa shule nyinginezo zenye mwelekeo wa nidhamu duni, kuna darasa la kina Mwakyambiki wanafanyaje kuupata ufaulu. Huo ni ushuhuda kwamba katika shule za kata au serikali kwa ujumla ufaulu ni jambo linalowezekana, muhuimu nui nidahamu na mikakati ya kitaaluma kwa watoto wetu.

# Vijana kunufaika 'toboa na kilimo'

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, amesema serikali ina mpango wa kuwaunganisha vijana na kilimo kupitia mfumo wa ulimaji kwa njia ya kitalu.

Mfumo huo watakaouanzisha utawakusanya vijana katika eneo moja la kilimo lenye miundombinu pamoja na kuwasaidia kupata masoko ya kuuza mazao yao.

Mavunde aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizindua kipindi cha Kilimo Kwanza, kitakachorushwa na Televisheni ya TV-E, kwa lengo la kuhamasisha kilimo na kutangaza sekta hiyo ndani na nje ya nchi.

Mavunde alisema kupitia mfumo huo, serikali itatenga Sh. bilioni tano kwa ajili ya kutekeleza mradi huo utakaofahamika kama 'Toboa na Kilimo'.

Aidha, Mavunde alisema vijana wengi wanashindwa kujiingiza kwenye sekta ya kilimo kutokana na dhana potofu walizojengewa tangu wanasoma kuwa, kilimo ni sehemu ya adhabu.

"Serikali inaendelea jitihada za kuwafanya Watanzania hasa vijana wakipende kilimo na kuwakomboa kiuchumi, tunafahamu pia wapo wanaojitahidi kulima lakini hawapati mazao toshelevu," alisema Mavunde.

Kadhalika alisema serikali inatumia mbinu za kisasa za kupima udongo, kufanya tafiti na kulima kisayansi ili kuwezesha wakulima kulima kilimo chenye tija.

Alieleza zaidi kuwa, kupitia kipindi hicho serikali itakitumia kueleza fursa mbalimbali na jitihada wanazofanya katika kuwawezesha wakulima kulima mazao yenye tija na yenye soko nje ya nchi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa EFM na TV-E, Francis Ciza, alisema kituo hicho kimejipanga kuwafungua vijana kufahamu namna gani wanaweza kunufaika kupitia kilimo.

Alisema vijana wengi wanaojihusisha na kilimo hawajivunii kazi hiyo na kwamba kupitia kipindi hicho watahamasisha na kuwajengea ujasiri vijana wengi kutambua umuhimu wa kilimo na namna ya kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema mpango mkakati ni kutafuta eneo zuri la kilimo ambalo mbali na wafanyakazi kuandaa vipindi vya kilimo kutakuwa na studio ili wafanyakazi wapate fursa ya kushiriki shughuli ya kilimo moja kwa moja.

# DC aagiza msako waliomuua askari wanyamapori

**Na Neema Hussein**, KATAVI

SERIKALI mkoani Katavi imeagiza kuwasaka na kukamata watu wanaodaiwa kuhusika na mauaji ya askari wa uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), James Karomba, aliyeuawa na watu wasiojulikana wakati akitekeleza majukumu yake.

Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Filberto Sanga, alitoa maagizo hayo juzi wakati akitoa salamu za pole kwa Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, familia na watumishi baada ya kumalizika ibada maalumu ya kuuaga mwili wa marehemu.

Sanga alisema vitendo hivyo havikubaliki na ni uvunjifu mkubwa wa sheria za nchi, hivyo akalaani mauaji hayo na kukemea vikali vitendo kama hivyo.

"Nafahamu vinaweza kuendelea na wale waliokuwa wamejipanga kufanya mengine nimesema hili liwe tukio la mwisho. Tutashirikiana na kamati za ulinzi na usalama zote wahusika wapatikane," alisema Sanga.

Naye Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa TAWA, Yusuph Kabange, alisema Karomba alikuwa mtumishi wa pori la akiba Rukwa liliko mkoani Katavi na alipatwa na umauti wakati akiongoza doria katika pori la akiba la Inyonga wilayani Mlele.

"Chanzo cha kifo chake ni kushambuliwa na wahalifu au majangili wakati anatekeleza majukumu yake Februari 17, 2022.

Aliajiriwa na serikali kama askari wa wanyamapori 2000 hadi 2016 alipohamishiwa katika Mamlaka ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na amekuwa kwenye utumishi huu kwa miaka 22," alisema Kabange.

Pia alisema tukio hilo linaonyesha uwapo wa watu ambao si wazalendo katika kulinda rasilimali za nchi ikiwamo wanyamapori na misitu.

Mwakilishi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Mkoa wa Katavi, Benedict Mbuya, alisema kifo cha Karomba ni mwendelezo wa matukio ya askari wa uhifadhi na watumishi wake kuendelea kuuawa na kujeruhiwa.

"Kwetu Katavi mwezi uliopita askari wetu alijeruhiwa kwa mkuki hadi sasa yuko Hospitali ya Bugando, Mwanza, amefanyiwa operesheni kubwa mbili. Rai yangu tusikate tamaa tuendelee kupambana," amesema Mbuya.

Nipashe ilizungumza kwa simu na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Alli Makame, na kubainisha kuwa wanawashikilia watu watatu wakidaiwa kuhusika na tukio hilo.

"Watu hao wako chini ya upelelezi. Wanaendelea kuhojiwa na mpango sasa kuna msako mkali sana dhidi ya wale wengine, hivyo tutaendelea kutoa taarifa mara kwa mara kuhusiana na hilo," alisema Kamanda Makame.

Karomba (46) ameacha mjane na watoto wawili na mwili wake umesafirishwa kupelekwa Ikoma, Serengeti mkoani Mara kwa maziko.

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF LINDI**

***(AT LINDI)***

**CRIMINAL CASE NO. 06 OF 2022**

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**WOCO OIL (T) LIMITED………………………………ACCUSED PERSON**

**To:**
Managing Director
WOCO Oil (T) Limited
Vijibweni Area, Kigamboni Municipality
Dar Es Salaam Region

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 7th day of March 2022 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 3rd day of Febr 2022

RESIDENT MAGISTRATE COURT KIBAHA PWANI ★ TANZANIA ★

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship
Date……………………………

216720002

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF LINDI**

***(AT LINDI)***

**CRIMINAL CASE NO. 06 OF 2022**

**THE REPUBLIC**

**VERSUS**

**WOCO OIL (T) LIMITED………………………………ACCUSED PERSON**

**To:**
The Manager
WOCO Oil (T) Limited
Kongowe Petrol Station
Kongowe Area, Kibaha District
Pwani Region

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 7th day of March 2022 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 3rd day of Febr 2022

……………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……………………………

Signature……………………………

Qualification/Relationship
Date……………………………

216720002



Kinamama wachimbaji na waongeza thamani ya madini wa kikundi cha Magonga cha Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoa wa Manyara, wakionyesha bidhaa zao za vito vya madini aina mbalimbali katika maonyesho ya mkutano wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania, katika kituo cha mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Saalam jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wanaohudumia watalii wapigwa msasa

**Na Amon Mtega, SONGEA**

CHUO cha Taifa cha Utalii, kimetoa mafunzo ya siku tano ya UVIKO-19 kwa zaidi ya wadau 140 wa huduma za utalii mkoani Ruvuma, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuwahudumia wageni wanapoenda kutembelea vivutio.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo, Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Sedoyeka, alisema mafunzo hayo yamefadhiliwa na mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na makabiliano dhidi ya UVIKO-19 kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii.

Alisema chuo hicho kimeamua kutoa mafunzo hayo kwa wadau wa utoaji wa huduma za utalii baada ya kubaini baadhi hawana weledi wa kutosha kuhusu ugonjwa huo wanapohudumia watalii.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Steven Ndaki, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alisema sekta ya utalii inatoa fursa nyingi ikiwamo ajira ndiyo maana mafunzo hayo yanatolewa.

Alisema katika kipindi cha janga kubwa la corona utalii uliyumba katika nchi mbalimbali hivyo kwa sasa inatakiwa kuitumia elimu ipasavyo ili kulinda watalii na jamii kwa ujumla.

Naye Ofisa Utalii katika Pori la Limbaramba, Maajabu Mbogo, alisema wanatarajia kuwa mafunzo hayo yataongeza watalii na mapato ya utalii.

Mmoja wa waliopatiwa mafunzo hayo kutoka Wilaya ya Nyasa, Bernad Lisambo, alisema mafunzo hayo yatawapa uzoefu wa kutoa huduma kwa wageni ambao ni watalii.

## KUMBUKUMBU



**Mzee VYOSEENA OMBENI MUMGHAMBA**

*Leo tarehe 24.02.2022, Mzee VYOSEENA OMBENI MUMGHAMBA, baba yetu, unatimiza miaka 20 tangu utwaliwe na BWANA tarehe 24.02.2002. MUNGU amilikiye wafu na wazima azidi kukuhifadhi.*

*Unakumbukwa sana na mke wako mpendwa Apendavyo John Mgonja; Watoto wako Violet, Ombeni na Naomba, Onike na Dr Kilonzo, Kaunda na Nambua, Timothy na Mercy, Nashanda na Ruth, Zera na Alex, Anna Nim pamoja na Lea na Daniel.*

*Pia wajukuu zako Caroline, Teddy na Emanuel, Ngana, Namhezi, Apendavyo, Hope, Angel, Vicky, Happy, Minael, Diana, Aaron, Erick, Nicholas, Osborn, Brayan, Vyoseena, Ryan, Kimario, Sareen na Joanna. Kadhalika Vitukuu Onike, Tassiana, Ivana na Owen.*

*UFU14: 13b "Heri wafu wafao katika BWANA tangu sasa, Naam, Asema Roho, wapate kupumzika taabu zao".*

***Uendelee kupumzika kwa amani. Amen.***

216720401

# Mvua yabomoa madaraja Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MVUA iliyonyesha siku mbili mfululizo, imebomoa madaraja matatu wilayani Ludewa mkoa wa Njombe, hivyo kusababisha shughuli za usafirishaji kutoka Ludewa kwenda Njombe kusimama.

Madaraja yaliyobomolewa ni Nyapinda njia panda ya kwenda Ibumi, daraja la Muhoro, daraja la chuma la Mhambalasi linalounganisha kata ya Mkomang'ombe na Ibumi pamoja daraja la Ludewa mjini kwenda Ludewa vijijini.

Akithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, alisema mvua hizo zimenyesha usiku juzi na jana.

Tsere aliwataka wananchi kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea kufanya jitihada za haraka kuweka madaraja ya muda na kuanza kuanza ujenzi wa madaraja ya kudumu.

Pia mkuu huyo wa wilaya alisema tayari amefanya mawasiliano na Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Njombe ili kuhakikisha hatua za haraka zinachukuliwa ili kunusuru maisha ya wanafunzi pamoja na wananchi katika maeneo hayo.

# CRB yataja sababu makandarasi kukimbia miradi

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

MAKANDARASI nchini wameshauriwa kuweka bei halisi kwenye zabuni za ujenzi badala ya kuweka gharama ndogo kwa lengo la kupata miradi ya ujenzi lakini mwisho wake wanakimbia kazi hizo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Consolata Ngimbwa, alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kuhusu usimamizi wa mikataba ya ujenzi.

Alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa wakiweka bei ndogo kwa lengo la kuwavutia watoa zabuni na kushinda miradi lakini mwisho wa siku kazi hizo zimekuwa zikiwatesa na wengi hushindwa kuzikamilisha na kukimbia.

"Tuwe makini tunapojaza zabuni tuweke bei halisi kwasababu unakuta mradi wa Sh. milioni 400 mtu anaweka milioni 200 sasa kweli huu mradi utaukamilisha kwa namna gani? Unachukua mradi ilimradi tu umepata mradi lakini unakukondesha na hata usingizi hupati sasa inakusaidia nini," alisema.

Aliwataka kwanza kusoma mikataba kwa makini kabla ya kuisaini na kama wakishindwa kuielewa wawatumie wataalamu badala ya kuingia kwenye mikataba hiyo na kuwasababishia hasara kubwa inayowaletea msongo wa mawazo.

Naye mwezeshaji wa semina hiyo, Mhandisi Emmanuel Kachuchuru, alisema makandarasi wengi nchini hawajiamini na wanashindwa kutetea haki zao zinapokiukwa na wateja wao sababu kubwa ikiwa ni kutokuwa na ufahamu wa haki hizo kwenye zabuni.

Alisema kukosa elimu kuhusu usimamizi wa miradi kumewafanya makandarasi wengi kuwa wanyonge na kuonewa na watoaji wa zabuni hivyo aliwataka kuchangamkia mafunzo kila yanapotokea ili waongeze ujuzi na uwezo wa kulinda haki zao.

"Wengine wanaogopa kudai haki zao kwa kuogopa kuwa siku nyingine hatapata kazi, kama ulipata kazi kwa uwezo wako huwezi kuogopa. Ila kama ulipewa kazi ya ujenzi kwa njia za rushwa huna nguvu ya kudai kwasababu aliyekupa atakushangaa umepata wapi nguvu hiyo," alisema.

Mara nyingi, alisema watoaji wa zabuni wamekuwa wakiwanyanyasa makandarasi ambao hawajui haki zao wala namna ya kuzitetea kwenye mikataba ya ujenzi tofauti na wale wenye uelewa na usimamizi wa mikataba ya ujenzi.

Aidha, alisema watoaji wa zabuni wamekuwa wakiwaogopa makandarasi wa kigeni kwani wanajua fika kwamba wanajua haki zao na wanauwezo mkubwa wa kuzidai kila zinapokiukwa.

"Niambieni lini mmesikia mkandarasi wa kigeni analalamika lalamika kama sisi? Ni kwasababu wanazijua na wana uwezo mkubwa wa kudai haki zao na vile vile hata hawa watoaji wa zabuni wanajua kwamba hawa ukiwagusa tu utapata shida, sasa na nyinyi mfike huko msikubali kuonewa," alisema.

Pia alisema asilimia 65 ya bajeti ya nchi inakwenda kwenye miradi ya ujenzi hivyo makandarasi wanapaswa kujua wajibu wao na kuisimamia kwa mujibu wa makubaliano ya kwenye mikataba wanayoingia na wateja wao.

"Miradi hii ya ujenzi ni mingi na inawapa fursa nyinyi ya kukua hivyo timizeni wajibu wenu kila mnapopata kazi na hakikisheni kila mtu anajua wajibu wake wewe na mwajiri wako ili mwisho wa siku kila mtu apate anachostahili," alisema.

# Wanawake wapewa jukumu magonjwa yasiyoambukiza

**Na Romana Mallya**

WANAWAKE wametakiwa kuwa walinzi wa kwanza wa familia dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa kuhakikisha kila siku wanaandaa mlo kamili ili kuzilinda na maradhi hayo ambayo matibabu yake huchukua muda mrefu na kutumia gharama.

Hayo yalisemwa juzi na Mbunge wa Malinyi, Antipas Mgungusi, wakati wa mafunzo ya siku mbili yaliyohusisha wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Kifua kikuu, dawa za kulevya na magonjwa yasiyoambukiza, wahariri wa vyombo vya habari na watu wanaoishi na magonjwa.

Mafunzo hayo yalishirikisha washiriki 64 na yaliandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA) na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia Mradi wa RECAP unaosimamiwa pia na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Lengo lake ni kusambaza muhtasari wa sera zinazolenga kukinga na kupambana na wimbi la magonjwa hayo ambayo ni pamoja na kisukari, saratani na shinikizo la damu na moyo. Akichangia katika mafunzo hayo, Mgungusi alisema wanawake wanatakiwa kuhakikisha familia zinapata chakula bora kisichokuwa na mafuta mengi, sukari na chumvi nyingi ili kuzilinda dhidi ya magonjwa hayo.

"Wanaume tunapotoka katika mihangaiko, ukifika nyumbani utakula chakula kilichoandaliwa mezani, hivyo basi kama mama ameandaa chakula hatarishi kwa afya utakula lakini pia kama ameandaa chakula chenye afya bora utakula.

"Ninawaomba wadau wa maendeleo waungane kutafuta mbinu zitakazowezesha kupunguza magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanapompata mtu kwenye familia hutumia muda mrefu na gharama kubwa kuyatibu na kusababisha familia nyingi kubaki maskini."

Mbunge huyo alisema gharama za kujikinga na maradhi hayo ni ndogo ikilinganishwa na matibabu kwa mtu anapoyapata na kusisitiza lazima watu wabadili mtindo wa maisha yao wa kila siku.

Meneja wa Elimu ya Afya kwa Umma ambaye pia ni Kaimu Meneja Kitengo cha magonjwa yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Bakari Magarawa alisema serikali inafanya juhudi kupambana na magonjwa hayo na kuwataka wadau nao waendelee kuhamasisha jamii namna ya kujikinga. Mhariri Mkuu wa Clouds Media Group na Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe alisema mafunzo hayo yamemfungua macho na kuona ukubwa wa tatizo hivyo kumpa jukumu kama mwandishi wa habari kuisaidia jamii kutoa taarifa za kuelimisha umma ili kupunguza vifo vinavyosababishwa na magonjwa yasiyoambukiza.

Joyce alisema waandishi wa habari wanapaswa kuisaidia jamii kwa kuielimisha namna ya kuepuka kupata magonjwa hayo kwa kufanya mazoezi, kula vyakula bora na kufuata mtindo bora wa maisha.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), akipokea machapisho ya nukta nundu kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, ikiwa ni msaada kwa Jumuiya ya Maendeleo kwa Wasioona Tanzania (TAB), jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka ukwepaji kodi uwe kigezo kuengua wagombea

**Na Mwandishi Wetu,** MUSOMA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, ameipongeza Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kuwafuata wafanyabiashara kwenye maeneo yao ya kazi ili kuwaelimisha masuala mbalimbali yanayohusu kodi, akisisitiza kutawajengea ari ya kulipa kodi kwa hiari.

Vilevile, ameshauri ukwepaji wa kulipa kodi uwe miongoni mwa vigezo vya kuwaengua wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi nchini.

Hapi alitoa kauli hiyo juzi wakati timu ya maofisa wa TRA ilipomtembelea ofisini kwake Musoma mjini kumpatia taarifa ya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango ambayo ilimalizika juzi mkoani humo.

Alisema kuna baadhi ya nchi wamefikia hatua anayegombea nafasi ya uongozi, historia yake ya ulipaji kodi inafuatiliwa na ikibainika aliwahi kukwepa kulipa kodi, anapoteza sifa ya kugombea, ikiwamo uchaguzi mkuu.

"Naamini kama nchi siku moja tufike mahali ambapo ili ugombee uongozi, historia nzuri ya ulipaji kodi iwe moja ya sifa, iwe fahari kuwa mimi ni mmoja wa walipakodi na ni sehemu ya maendeleo ya taifa," alisema Hapi.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, aliushukuru uongozi wa Mkoa wa Mara, viongozi wa wafanyabiashara pamoja na wafanyabiashara wote kwa ushirikiano walioutoa kwa timu ya maofisa wa TRA waliofanya kampeni hiyo mkoani humo na kufanikisha kuwafikia jumla ya wafanyabiashara 4,014.

"Katika zoezi hili, tumefikia jumla ya wafanyabiashara 4,014 ambapo Wilaya ya Tarime tumefikia wafanyabiashara 2,088, Bunda 1,126 na Musoma Mjini tumefikia wafanyabiashara 800," alibainisha Kayombo.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, Kilimo na Viwanda (TCCIA) Mkoa wa Mara, Boniphace Ndengo, aliishukuru TRA kwa kutoa elimu mkoani humo ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha mabadiliko ya sheria za kodi kila zinapopitishwa na Bunge.

Wafanyabiashara wa Wilaya ya Musoma mkoani humo kwa nyakati tofauti walisifia kitendo cha TRA kupita mlango kwa mlango kuwapatia elimu na kusema kwamba wameepushwa na makosa yanayotokana na kutokuwa na uelewa wa masuala ya kodi.

Nyangaro Mseti ni mfanyabiashara wa Musoma Mjini ambaye alisema utaratibu huo unawasaidia kupata muda wa kutosha kuuliza maswali na kupatiwa ufafanuzi kuhusu kero mbalimbali za kikodi zinazowakabili.

Mfanyabiashara mwingine Eunice Julius alisema awali walikuwa wakiitwa eneo moja kwa ajili ya kuelimishwa juu ya masuala mbalimbali ya kodi, lakini baadhi yao walikuwa hawaendi kwa sababu walishindwa kufunga biashara wakihofia kukosa mauzo.

"Sasa mnatufuata na kutufundisha, akija mteja mnasubiri mpaka nimalize kumhudumia kisha mnaendelea, kwa kweli utaratibu huu ni mzuri sana maana elimu tunapata na mauzo hayapungui ndiyo maana naomba mwendelee tena, mje mara kwa mara," alisema Julius.

# GGML yatoa milioni 90/- mkutano wa madini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji wa madini ya dhahabu mkoani Geita (GGML) imetoa msaada wa Sh. milioni 90 kudhamini mkutano wa nne wa uwekezaji wa madini mwaka huu unaofanyika jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini ulifanyika kwa muda wa siku tatu hadi jana katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Mwalimu Julius Nyerere ulioko jijini Dar es Salaam.

Aidha, msaada huo wa GGML ambao unaifanya kampuni hiyo kuwa mfadhili mkuu unajumuisha ukodishaji ukumbi katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kwa muda wote wa mkutano huo pamoja na matangazo yanayohusu hafla hiyo.

Akizungumzia udhamini wa kampuni hiyo mwaka huu jana jijini Dar es Salaam, Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo, aliishukuru serikali kuonesha dhamira ya wazi katika kuinua sekta ya madini.

Pia ameahidi kuwa kampuni hiyo itaendelea kuzingatia sheria na taratibu na kuendelea kuwa moja ya inayoongoza kwa kulipa kodi na mapato mbalimbali ya Serikali.

"Sekta ya madini imenufaika kutokana na ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa miaka kadhaa. Katika kukuza maendeleo, GGML imejipanga kuendelea kushirikiana na serikali ili kuleta manufaa kwa pande zote mbili pamoja na wadau wengine," alisema.

Aliongeza kuwa ana matumaini makubwa kuwa Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sekta ya madini nchini Tanzania.

"Malengo yetu yanaendana na yale ya serikali kwamba sekta ya madini inapaswa kuchangia angalau asilimia 10 kwenye pato la taifa (GDP) ifikapo mwaka 2025 na pia kuleta manufaa mapana kwa jamii," alisema.

Katika hafla kama hiyo mwaka jana, GGML ilitambuliwa na serikali kama kampuni iliyofanya vizuri zaidi katika sekta ya madini nchini Tanzania kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

GGML ilishinda tuzo hiyo baada ya kupata alama za juu zaidi katika kipengele cha uwajibikaji wa kampuni kwa jamii, mazingira na usalama, kampuni inayoongoza kwa kulipa kodi na mapato ya serikali na kampuni inayoongoza kwa kutoa biashara kwa kampuni za ndani.

# Miradi ya umwagiliaji yadaiwa kukosa tija

**Na Gideon Mwakanosya,**
NAMTUMBO

MTANDAO wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), umedai miradi ya umwagiliaji iliyoko wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma haina tija kwa wakulima kwa kuwa haizalishi kama ilivyotarajiwa na kuwaneemesha wakulima katika maeneo yaliyojenga miradi hiyo.

Mratibu wa ufuatiliaji wa rasilimali za umma kutoka MVIWATA katika sekta ya kilimo wilayani Namtumbo, Shifla Ally, katika taarifa yake alisema Wilaya ya Namtumbo ina miradi 14 ya umwagiliaji na katika miradi hiyo ni kiwango kidogo kinachofanyiwa kazi hali inayofanya kutoonyesha tija kwa wakulima tofauti na malengo ya serikali.

Shifla Ally alidai walifuatilia miradi ya umwagiliaji katika Kata ya Kitanda, Limamu na Kata ya Ligera ambapo pamoja na changamoto zingine walibaini kutokuwapo na usimamizi unaotokana na walengwa wa mradi kutoona faida ya miradi hiyo kwa kuwa hawakushirikishwa toka awali na kuitazama miradi kama sio yao.

Jovinari Mhagama aliyekuwa mwenyekiti wa skimu ya umwagiliaji ya Njomlole alisema kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi huo hapakuwa na uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji kwa wakulima na viongozi wa serikali katika kupanga na kutekeleza mradi huo ndio maana wananchi au wakulima hawaoni umuhimu wa miradi hiyo kwa kutowashirikisha toka awali ili waione miradi hiyo ni ya kwao.

Ofisa Umwagiliaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, Eleuter Mndendemi, alisema kuwa kati ya miradi 14 ya umwagiliaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo hakuna mradi wowote uliokamilika bali wakulima wachache ndio wanaonufaika na wengine wamekosa kutokana na kutokamilika kwa miundombinu hiyo ya umwagiliaji.

Mnung'a Shaibu , Mkurugenzi wa Millennium Art Group alitoa mwongozo wa utekelezaji wa miradi ya serikali mambo yanayopaswa kuzingatia ili miradi hiyo iwe endelevu na kuwa na tija katika jamii.

Alitaja suala la uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji katika utekelezaji wa miradi utawafanya wananchi kufuatilia na kushirikishana katika ngazi mbalimbali za maendeleo ya miradi yao ili waweze kuilinda na kuiendeleza baada ya mradi kukamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma, Dk. Julius Kenneth Ningu, pamoja na mambo mengine aliwataka wakulima kujikita katika kilimo cha mazao mchanganyiko ili kujipatia kipato na changamoto zilizojitokeza katika skimu za umwagiliaji zitafanyiwa kazi alisema mkuu wa wilaya huyo.

MVIWATA inatekeleza mradi wa utawala bora na ufuatiliaji wa rasilimali za umma katika wilaya ya Namtumbo likiwa na lengo la kuimarisha mamlaka za serikali za mitaa ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuongeza uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji kwa wananchi ili miradi inayotekelezwa ilete tija kwa wananchi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (katikati), akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dare s Salaam jana, kuhusu mafanikio ya benki hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, Afia Sigge na Kaimu Mkurugenzi wa Fedha, Goodchance Haron. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aiagiza TFS kasi upandaji miti

**Na Neema Hussein,** RUVUMA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kutumia mvua zinazoendelea kunyesha kuongeza kasi ya kupanda miti katika maeneo ya wazi yaliyoathiriwa na shughuli za kibinadamu katika maeneo mbalimbali mkoani humo.

Ibuge alitoa agizo hilo wakati akizindua mpango wa upandaji miti kimkoa uliofanyika katika Kijiji cha Mwande Kata ya Mateteleka Halmashauri ya Madaba wilayani Songea.

Aidha, Brigedia Ibuge, amewaonya wananchi kuacha tabia mbaya ya kuchoma kwa makusudi miti inayopandwa na serikali kupitia TFS kwa kuwa hiyo ni sehemu ya miradi inayoliingizia Taifa fedha nyingi.

Alisema, kuchoma moto kwa makusudi mashamba ya miti ni ushamba na kamwe serikali haitawavumilia hata kidogo watu hao kwa sababu serikali inatumia fedha nyingi kuandaa mashamba hayo na amewataka wananchi kuheshimu uwekezaji huo.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa Mkoa aliipongeza TFS kwa kupanda miti 700,000 tangu mvua za masika zilipoanza kunyesha katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Hata hivyo, aliomba kazi hiyo iwashirikishe wananchi na kutoa ushauri kuhusu miti sahihi inayopaswa kupandwa, badala ya kuacha wananchi wanapanda miti holela na matokeo yake kukauka kutokana na kupandwa sehemu zisizo sahihi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, serikali haiwezi kutekeleza kila jambo peke yake, bali wananchi ni muhimu washirikishwe na washiriki katika shughuli zote za maendeleo kwani hatua hiyo itasaidia kulinda miradi hiyo kwa kuwa wataiona ni yao. Wakala wa TFS ya Kusini, Manyisye Mpokigwa, alisema TFS ina jukumu la kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinalindwa kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwamo Wakala wa Huduma za Maji (RUWASA) kwa kupanda miti katika maeneo yote yaliyoathirika na shughuli za kibinadamu.

Naye Meneja wa shamba la miti Wino Glory Kasmir alisema, wamefanikiwa kupanda miti 700,000 katika vijiji na maeneo ya ofisi za serikali kwa ajili ya kurudisha maeneo yaliyoathirika katika hali yake ya asili.

# Dk. Mpango akunwa na mchango wa NMB madini

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, ameipongeza Benki ya NMB, kwa mchango mkubwa inaotoa katika kustawisha Sekta ya Madini Tanzania, ilitumia zaidi ya Sh. bilioni 70 kati ya Sh. bilioni 240 za mikopo nafuu kwa wadau walioko kwenye mnyororo wa thamani wa sekta hiyo kwa miaka miwili.

Alitoa pongezi hizo juzi alipotembelea banda la NMB, kabla ya kuhutubia Kongamano la Kimataifa la Uwekezaji katika Sekta ya Madini, linalofanyika kwa siku mbili jijini Dar es Salaam.

Kupitia kongamano hilo, lililofunguliwa na Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta hiyo wa ndani na nje ya nchi, NMB kupitia kwa Mkuu wa Idara ya Biashara, Alex Mgeni, alisema benki yake tayari imetumia zaidi ya Sh. bilioni 70 kutoa mikopo kwa wadau wa madini na kwamba mwaka huu wanatarajia kutumia Sh. bilioni 240 kuwawezesha wachimbaji wadogo.

Mgeni alisema katika kuhudumia wachimbaji wadogo, moja ya changamoto walizokutana nazo ni pamoja na ukosefu wa taarifa sahihi za wadau hao, lakini uanzishwaji wa Klabu ya Madini sambamba na ushirikiano na Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), Chemba ya Madini (TCM), Stamico na ofisi za madini mikoa, wamefanikiwa kupunguza mkwamo uliotokana na hilo.

"Tunaishukuru serikali na taasisi zake kwa namna inavyotuwezesha katika kuwahudumia wadau wa sekta ya madini nchini na tunaahidi kuwafikia kila mmoja, ndio maana tuna kiasi kikubwa cha pesa kinachofikia bilioni 240 mwaka huu, pamoja na elimu ya fedha na utunzaji kumbukumbu zao kwa ustawi wa biashara zao na Maendeleo Endelevu ya Sekta nzima, wachimbaji na Taifa kwa ujumla," alisema Mgeni.

Dk. Mpango alivutiwa na maelezo hayo, ambako aliipongeza NMB kwa uwezeshaji huo na kuitaka ihakikishe inayafikia makundi yote, hasa ya vijana na kuwashika mkono kwa kuwaonyesha fursa zilizoko na thamani yake, ili kuharakisha maendeleo yao nakuchangia pato la taifa lao.

"Sasa ongezeni kasi kuwafundisha vijana wazitambue fursa hizi. Vijana Tanzania wana mawazo mazuri sana ya kuboresha maisha yao, ila changamoto yao kubwa ni ukosefu wa mitaji.

"Kwa hiyo mkatoke mkawafundishe vijana wetu wa kike na wa kiume kote nchini, ili wajue kwamba fursa hizi zipo, na zinaweza sio tu kuboresha maisha yao, bali pia wakawa sehemu ya wachangiaji wa pato la Taifa lao," alisema Dk. Mpango.


ama
ALHAMISI FEBRUARI 24, 2022
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 14

Ugali mahindi lishe unavyoboresha afya ya mwili na akili ya binadamu


Ukurasa 13

Ethiopia imeanza kuzalisha umeme Mto Nile baada msuguano miaka 10


Ukurasa 12

**DUNI MACHANO HAJI:**
**Mjuzi wa dawa asili anayegeuka bingwa kukabili kunguni Zanzibar**

# Kasi kifafa inavyounganishwa na kukithiri mikasa ya ajali bodaboda

**Na Yasmine Protace,**

MKURANGA

UGONJWA wa kifafa unatajwa kusababishwa na matukio ya aina mbalimbali, ikiwamo ajali za barabarani.

Baadhi ya watu wanadhani unawapata watoto wadogo pekee, kumbe kinyume chake inagusa kada ya umri wowote, wadogo na watu wazima.

Inatajwa kuwapo kwa aina nyingi za kifafa, ikianzia kwenye mimba, wapo wanaotetemeka mikono, wanaoanguka chini na kuzubaa, pia hali ya degedege kwa kuwa na homa kali kwa mtoto.

Muuguzi Bingwa wa Magonjwa ya Akili, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Jane Mwenda, anasema ajali za bodaboda hutokea na kusababisha mtu kuumia kichwa, hata zinamsababishia kifafa katika siku za baadae.

Anasema, mtu anaweza ukaumia kichwani na baadaye kati ya wiki mbili na nne, kichwa kinaanza kumsumbua na hata anapofikishwa katika vipimo anakutwa ana degedege.

Hapo anatoa tahadhari kwa wazazi na walezi wanaowapiga watoto vichwani, huwasababishia baadae kupata degedege.

Jane anasema, pia ni kundi linalohusisha wale ambao mikono yao inatetemeka muda mrefu hata wakishika kitu, inafikia hatua inawaponyoka na kuanguka au wanazubaa, nao wanakutwa




Mwendesha bodaboda akiwa na abiria wake. **PICHA: MTANDAO**

wanasumbuliwa na degedege.

Anasema kinachotakiwa mtu akiwa na dalili mbaya katika mwili kama vile ya kupatwa na ajali, muhimu ni kupatiwa huduma ya kwanza asifikie hatua akapatwa na degedege.

Muuguzi huyo anatoa angalizo kwamba kwa wanaotumia usafiri wa bodaboda na wanakataa kuvaa kofia ngumu, wajue inapotokea ajali nao wakaumia vichwani, hatari iliyo mbele yao ni kuumizwa ubongo hata kupatwa na madhara hayo tajwa.

Jane anafafanua kuwa degedege inatibika na kupona, tiba yake ni mgonjwa kuanza kutumia dawa na baadae akiendelea vizuri, anapunguziwa siku za kumeza dawa na mwisho wake anaimarika kabisa kiafya.

Umoja wa Wazazi wenye Kifafa Tanzania (UWAKITA) wilayani Mkuranga mkoani Pwani, wanaitaka Polisi kikosi cha Usalama Barabarani , Mkoani Pwani, kuwachukulia hatua za kisheria madereva hasa wa bodaboda na abiria wasiovaa kofia ngumu, ili kupunguza ongezeko la wagonjwa wa kifafa.

Akizungumza katika Siku ya Kifafa Duniani, iliyofanyika kiwilaya katika Shule ya Msingi Kisemvule, Mwenyekiti wa umoja huo, Richard Shillo, anasema jamii inapaswa kujua ugonjwa ni zao la sababu, zikiwamo ajali zinazoharibu ubongo.

"Ugonjwa wa kifafa unatibika, unatibika kama mtu kapata ugonjwa huo anapatiwa vipimo na kuanza kupata dawa kuendana na tatizo lake na kadri anavyoenda hospitali, anapochunguzwa maendeleo ya ugonjwa wake anaweza kuanza kupunguziwa matumizi ya dawa," anasema.

Diwani wa Kata ya Vikindu, Mohamed Mahundu anaupongeza umoja huo kwa kuichagua kata yake kufanyia halfa hiyo, akiomba ipatiwe ekari 10 kati ya 40, wanazomiliki eneo la Kisemvule, ili awashirikishe wadau na madiwani wenzake kujenga madarasa maalumu na mabweni kwa ajili ya wanafunzi wenye kifafa.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Omary Makunge, ambaye pia mwanachama wa umoja huo, anawaomba wenyeviti wenzake kutumia mikutano yao kuelimisha madhara ya ajali za bodaboda yanayochangia jamii kupata kifafa.

Pia, anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwaletea mamilioni ya fedha za UVIKO 19 katika kunufaisha elimu, afya na miundombinu yake, huku akitaka kutupiwe macho sekta ya elimu katika kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wenye ugonjwa wa kifafa.

MAZINGIRA

DUNI MACHANO HAJI:

# Mjuzi wa dawa asili anayegeuka bingwa kukabili kunguni Z'bar

## • Atamba kumaliza kilio cha vijiji • Tenda ofisini nako apigiwa saluti • Mdudu wa vyekundu, njano hapana

**Na Romana Mallya**

DUNI Machano Haji, ni mwenyeji wa Unguja sehemu ya Tanzania inayoundwa na Visiwa vya Unguja na Pemba na ya Pwani ya Afrika Mashariki, akiwa na uamuzi kutaka kusafiri kwa boti akitumia takriban saa moja hadi Dar es Salaam, kuinadi dawa yake kuua mdudu sugu kunguni.

Kunguni au 'bedbugs' ni mdudu mwenye uwezo mkubwa wa kustahimili hatari dhidi ya maisha yake na utafiti unaonyesha sumu ya kuua viumbe huwa inamuimarisha zaidi, badala ya kumuua.

Je inakuwaje mtaalamu Duni anafanikiwa kuwasambaratisha? Ndio unapoanzia mjadala na Nipashe na mzalishji huyo, akiwa mgeni maalum katika ofisi zake Mikocheni, Dar es Salaam wiki iliyopita.

Itakumbukwa Julai Mosi mwaka 2019, gazeti hili lilichapisha Ripoti Maalum ya kunguni yenye kichwa cha habari 'Siri ugumu kunguni kufa, wanavyotesa familia nyingi.'

Duni anasema dawa zake hazipambani na kunguni pekee, pia wadudu wote kero kwa familia akijisifu ameweza kumaliza tatizo la kunguni lililokuwa likiwasumbua kwa muda mrefu wanakijiji wa Charawe na Ukongoroni, Unguja.

"Baada ya kupulizia dawa kunguni wote walikufa na mazalia yao. Hii ilinipa sifa kubwa, kwa sababu wanakijiji walihojiwa na moja ya redio visiwani Zanzibar, wakaeleza namna walivyoteseka kwa muda mrefu na tatizo la wadudu hawa ambao wamekwisha baada ya kuwapulizia dawa yangu," anasema.

Duni anasema baada ya kazi hiyo, sifa zikaendelea kuenea na vijiji vya Bubwini, Nungwi, Matemwe, Kizimkazi, Mkunguni, Kizimkazi Dimbini na Miembeni, vyote vya Unguja ambako walimuita kutatua tatizo hilo.

Mbinu anayotumia kujitangaza anaitaja ni kupita mtaani akipaza sauti kwa wananchi namna uwezo wa dawa hiyo anayoitengeneza inamudu kuwaangamiza wadudu wasumbufu kama kunguni, utitiri, viroboto, mchwa na mende.

"Nikishajitangaza mwenye tatizo akisikia ananiita, na ninachofanya nitaviweka vitu vya nyumba kwenye mpangilio mzuri, ili nikipuliza dawa kila eneo lenye tatizo niweze kuangamiza na mazalia yake.



Duni Machano Haji, mtaalamu wa kutengeneza dawa za kunguni. Akionyesha nyaraka zinazoidhinisha uhalali wa uzalishaji na biashara zake, Zanzibar, alipokuwa katika ofisi ya Nipashe. Picha ndogo; mdudu kunguni. **PICHA: ROMANA MALLYA**

> **"Ninawaomba serikali wakati wowote kama watakuwa na tatizo la wadudu wasumbufu kama mende, kunguni na wengine waniite niwasaidie.**

"Nilikwenda hoteli moja (anaitaja) walikuwa na mende wadogo wengi jikoni na walishindwa kuwadhibiti wasiendelee kuzaliana. Basi nilipofika niliwapulizia dawa na kuwaondoa wote," anaeleza.

### MZIZI WAKE

Duni anasema aliamua kujikita katika kutengeneza na kuuza dawa hizo, kwa ujuzi alioupata tangu akiwa mdogo, akieleza: "Nilijikita rasmi kwenye biashara hii ya dawa hizi mwishoni mwa mwaka 2018. Ninatumia mitishamba inayopatikana kwenye mazingira yetu."

Anasema utundu wa kuchanganya dawa zake za asili umetokana na wana familia, pia babu yake kuwa mtaaluma wa dawa aina hizo, vilevile matibabu ya mwanadamu.

"Ninakumbuka niliwahi kuugua ugonjwa wa homa ya manjano nikiwa Tanga basi nikapelekwa Zanzibar na babu alipopata taarifa, aliwaagiza ndugu zangu wachukue dawa (bila kuzitaja) wakazichanganya nikaletewa hospitali.

"Na nilipotumia ndani ya siku tatu macho yakabadilika nikapona. Madaktari wakawa wanaulizana nimetumia dawa gani, ndugu zangu wakawajibu hizo za hospitali," anasimulia na hata mtoto wake hivi karibuni aliugua tatizo hilo na alipomtengenezea dawa hiyo, alipona na kuruhusiwa kwenda nyumbani.

### SIFA YA KUNGUNI

Duni anasema ubora wa dawa yake umemuwezesha kupata usajili wa serikali, ingawa pia analalamika kupata soko la bidhaa zake. Anafafanua: "Dawa zangu zinatambulika na taasisi za serikali lakini ugumu nilio nao ni upataji wa kazi.

"Ninawaomba serikali wakati wowote kama watakuwa na tatizo la wadudu wasumbufu kama mende, kunguni na wengine waniite niwasaidie. Nilifanikiwa kufanya kazi na taasisi moja ya serikali (anaitaja).

"Walikuwa na tatizo la mchwa, nilipiga dawa yangu na sasa wapo salama. Wito wangu kwa serikali wasitudharau sisi wadogo."

"Mchakato wa kutambuliwa, nilikwenda na dawa yangu kwa Msajili ikiwa kwenye chupa wakaifanyia uchunguzi kama ina madhara kwa binadamu au la, wakagundua haina madhara," anasema.

Duni ana hoja kwamba kwa serikali, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla wanaosumbuliwa na kunguni, hakuna usugu katika kuwaangamiza.

Anamtafsiri kwa wasiomjua kwamba ni mdogo mwenye miguu sita, kulia mitatu na kushoto idadi kama hiyo na hawezi kuruka kama mende, hutambaa chakula chake ni damu na ndiyo maana msumbufu kwa mwanadamu.

Duni anawaainisha kwamba wapo wa aina nyingi, akitaja wanaouma popo pekee na waliobobea kwa binadamu.

Anawataja wadudu hao kihistoria wamedumu miaka mingi, ila kampeni maalumu ilifanikisha kuwamaliza katika nchi zilizoendelea kama vile Marekani na ukanda wa Ulaya wakamalizwa mwaka 1940. Hata hivyo mwaka 1995 wanatajwa walirudi wapya.

Sababu za kurudi kwao, inatajwa dawa za kuwakabili ziliwatengenezea usugu, hivyo kukosekana nguvu za kuwaangamiza zikapigwa marufuku, pia dawa hizo zikithibitika zina madhara kwa binadamu.

Mdudu huyo hutaga mayai kila siku kuanzia moja hadi matano na baada ya yai, anaanzia mdogo zaidi wastani wa milimita 1.5 kisha hukua hatua kwa hatua hadi anafikia kuwa kunguni kamili.

Mara nyingi amekuwa na tabia ya kujificha hasa nyakati za mchana kwenye maeneo ambayo siyo rahisi kugundulika na hushamiri na kuonyesha makeke yao nyakati za usiku watu wakiwa wamelala.

Watafiti wanamchambua mdudu huyo kama ilivyo kwa binadamu, ana uchaguzi wa rangi wazipendazo zaidi ni nyeusi na nyekundu na wasizozipenda ni kijani na njano.

Duni, mzaliwa wa Wilaya ya Kaskazini Unguja, anasema kupitia dawa yake, amevisaidia vijiji tisa visiwani humo, hoteli na meli moja zilizopata madhila ya kuingiliwa na kunguni, pia wadudu wengineo, hata wakaangukia usumbufu.

"Ni kweli kunguni ni tatizo kubwa kwa familia nyingi, kwa sababu kumwangamiza kunahitaji utaalamu na dawa ambayo itamaliza mazalia yake yote, ili nyumba ibaki salama. Usipoangamiza mazalia baada ya muda hurejea," anasema.

Kuhusu elimu yake, Duni anasema alisoma katika Shule ya Msingi Mkwajuni na baadae Potoa ambako hakuvuka kusonga katika elimu ya sekondari na hapo akajiunga na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM).

Anasema hapo alikuwa na fani ya kucheza soka, ambako alipewa fursa ya kujiendeleza katika Chuo cha Ufundi Mbweni.

MAZINGIRA

MRADI UNAOWEKA REKODI...

# Ethiopia imeanza kuzalisha umeme Mto Nile baada msuguano miaka 10

• Yatenguliwa haki ya Misri tangu 1929

**Na Mwandishi Wetu**



Namna ulivyo mradi mpya wa kuzalisha umeme katika Mto Nile, nchini Ethiopia. **PICHA: MTANDAO**

BWAWA la kuzalisha umeme lililobeba utata kwa muongo mmoja, kuhusisha uhalali wa Ethiopia kwenye mto wa Nile, lilianza kuzalisha umeme kwa mara ya kwanza Jumapili iliyopita.

Bwawa hilo lenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 4.2 au sawa na wastani wa Sh. Trilioni 10, magharibi mwa eneo la Benishangul-Gumuz, ambako kumekuwa chanzo cha mzozo kati ya Ethiopia, Misri na Sudan tangu kuanza ujenzi mwaka 2011.

Hofu ya Sudan na Misri, ni kwamba mradi huo unaweza kupunguza sehemu ya maji wayapatayo kutoka Mto Nile, huku Ethiopia ikisisitiza kuwa bwawa hilo ni muhimu kwa maendeleo yake.

Bwawa linaloitwa Grand Ethiopian Renaissance Dam (Gerd) ni mradi mkubwa zaidi wa umeme wa maji barani Afrika, ikitarajiwa kuzalisha zaidi ya megawati 5,000 za umeme, hivyo kuongeza pato la taifa la umeme maradufu itakapokamilika na kwa sasa ikifikia asilimia 83.9.

Katika hafla ya ufunguzi wikiendi iliyopita Jumapili, Abiy Ahmed alizuru katika kituo cha kuzalisha umeme katika bwawa hilo na kubofya vitufe kadhaa ambavyo vilianzisha utayarishaji wa uzalishaji, kwa mujibu wa maofisa nchini humo.

Ujenzi wa bwawa hilo umesababisha mfarakano kati ya Misri na Sudan, pale serikali ya Ethiopia inapoelekeza maji ya Nile kujaza hifadhi kubwa nyuma ya bwawa hilo.

Misri, ambayo iko chini ya mto inategemea Mto Nile kuipatia maji ya kutumia na imekuwa ikihofu itaathiri viwango vya maji yanayoingia nchini humo.

Hivyo, hapo Misri imekuwa na dai la uhakikisho kuwapo kiasi cha maji yanayoingia huko, huku Ethiopia ikisita kuhusishwa na takwimu za maji yanayoingia katika mkondo wa mradi wa umeme.

Sudan, ni kama Misri ikionyesha ina wasiwasi kuhusu bwawa hilo litakavyoathiri viwango vyake vya maji na mwaka jana. Sudan ilieleza kushangazwa na Ethiopia kufunga vituo vitatu kati ya vinne vya kuelekeza maji, hata kusababisha viwango vya chini vya maji chini ya mkondo.

Hiyo ilivitatiza vituo vya kusukuma maji vya Sudan kwa ajili ya umwagiliaji na usambazaji wa maji katika miji yake.

Nchi zote mbili zimekuwa zikigombea makubaliano na Ethiopia juu ya kujaza na uendeshaji wa bwawa hilo, lakini mazungumzo yameshindwa kufanikiwa.

> **Tuna mpango wa kuanza kujaza bwawa hilo katika msimu ujao wa mvua (mwaka 2019) na tutaanza kuendesha mitambo miwili ya umeme kuanzia mwezi Desemba mwaka 2020.**

Kimsingi, kabla ya mradi kuanza Ethiopia imekuwa ikikabiliwa na tatizo la uhaba wa umeme, kwa kiwango zaidi ya asilimia 65 ya wananchi wake hawajaunganishiwa umeme, ikiwa na matarajio ziada ya umeme huo itauzwa kwa nchi za jirani.

Aidha, nchi hiyo inakosoa namna mataifa ya kigeni yanavyoingilia ujenzi huo kukiwapo matarajio mataifa ya Sudan, Sudan Kusini, Kenya, Djibouti na Eritrea yanatarajiwa kunufaika na mradi wa bwawa, ambao gharama zake hazitegemei ufadhili wa nje.

Sudan inatarajiwa kunufaika nao katika namna ya kujiepusha na mafuriko yaliyokuwa yanawakabili, hasa kila kipindi kati ya mwezi Agosti na Septemba.

### WALIKOTOKEA

Miaka miwili iliyopita kulitolewa taarifa kuhusu uchambuzi wa mzozo huo ulioanza mwaka 2011, ikikadiriwa asilimia 85 ya maji yanayotiririka yanatoka Mto Nile, hata kuna wakati Marekani iliingilia kati kusuluhisha na kukawapo maelewano.

Mzizi wa kinyongo cha Misri, inayotegemea maji ya mto Nile kwa asilimia 80 imekuwa na hofu kuwa bwawa hilo litaathiri mfumo wa usambazaji maji na kuifanya Ethiopia kuwa na mamlaka juu ya usambazaji maji ya mto huo mkubwa Afrika.




Ramani safari ya maji ya Mto Nile.

Mtazamo wa malalamiko ni kituo hicho cha kuzalisha umeme kwamba hakitatumia maji mengi, bali bwawa hilo linalojengwa na Ethiopia, litaathiri kwa kiwango kikubwa kasi ya mtiririko wa maji.

"Tuna mpango wa kuanza kujaza bwawa hilo katika msimu ujao wa mvua (mwaka 2019) na tutaanza kuendesha mitambo miwili ya umeme kuanzia mwezi Desemba mwaka 2020," ni matamshi ya Waziri wa Maji wa Ethiopia wakati huo 2019, Seleshi Bekeli.

Misri ikatolea ufafanuzi kwa maoni kwamba, ingechukua miaka 10 mto kurejea kawaida kutokana na athari za mradi katika mfumo wa usambazaji wa maji, hasa kwa hatua za awali.

### GADHABU YA MISRI

Misri inategemea maji ya Mto Nile kwa asilimia 85 kihistoria, inayategemea kwa kiwango kikubwa maji hayo, hivyo chochote kinapoathirika kuna tafsiri ya athari kitaifa.

Ikirejewa makubaliano ya mwaka 1929, yalizipa Misri na Sudan haki ya mto wote zama hizo za utawala wa kikoloni, Misri ikipewa kura turufu dhidi ya mradi wowote utakaoendeshwa katika hali itakayogundulika kuwa haifai.

Ethiopia inapinga hakuna haja ya kuendelea kufungwa na makubaliano yenye miaka 82 hadi mradi ulipoanza kujengwa mwaka 2011 bila ya kushauriana na Misri.

Mto Nile unasambaza maji katika mji wa Aswan Kusini mwa Misri, umbali wa maili 570 kutoka mji mkuu wa Cairo na Rais wa Misri Abdul Fattah al-Sisi, akanukuliwa mwaka huo 2019, kwamba ushawishi wa kisiasa hauathiri mfumo wa mto huo.

Nchi za Kaskazini mwa Afrika na majirani wa Misri wanaeleza shaka yao kwenye Ziwa Nasser, inayoitengenezea umeme Misri.

Vilevile, mradi huo wa usafirishaji unatajwa uko hatarini kuathirika, pale kiwango cha maji kitakaposhuka na kuwaathiri wakulima wanaotegemea maji hayo kwa kilimo cha umwagiliaji.

### ILIAMBATANA NA VITA?

Mwaka 2013 kulikuwapo ripoti za siri zinazoonyesha wanasiasa wa Misri wanapendekeza kuwapo mapigano dhidi ya Ethiopia, katika juhudi za kupinga ujenzi wa bwawa hilo.

INAENDELEA UK.14

AFYA

# Ugali mahindi lishe unavyoboresha afya ya mwili na akili ya binadamu

**Na Dotto Kahindi**



Wema Msambusi, akiwa na familia yake wakibariki chakula kabla ya kula mchana; ugali wa mahindi lishe, na mboga nyinginezo. **PICHA: DOTTO KAHINDI**

NI mchana wenye jua kali linaloambatana na baridi yenye upepo mkali, zikiwa zimesalia dakika chache tu kengele ya shule igongwe kuwaruhusu wanafunzi kurejea majumbani.

Mwanamama huyo mwenye umbo nene kiasi na mwenye uso uliojawa tabasamu, ameketi jikoni huku akichekecha unga wa mahindi lishe tayari kusonga ugali.

Sufuria kubwa la ugali liko juu ya mafiga, moto umekolea na maji yanachemka yakiusubiri unga ili yafunge ndoa na kuzaa ugali.

Mboga za kuambatana na ugali tayari zimeshapikwa na sasa zimewekwa pembeni kuitazama ndoa ya unga na maji, zikimsubiri mtoto ugali ili kumpatia matunzo.

"Kila ikifika saa nane mchana, ni lazima chakula kiwe tayari mezani ili wanangu wanapofika tu kutoka shule, wafikie kula chakula," ni maneno ya mwanamama Wema Msambusi, mkazi wa Kijiji cha Mangalali, mkoani Iringa.

Mbali na ukulima huo, Wema pia ni mama wa watoto sita wanaomtegemea kamili katika mahitaji yao kila siku. Shambani anajishughulisha na kilimo cha mazao mengi, huku mahindi lishe yakionekana kuleta tija kwake na familia kiuchumi, kiafya, hata kielimu. Wema pia ni Katibu wa Kikundi cha Kuweka Akiba na Kukopa (VICOBA) cha Amani, kinachoendesha kilimo biashara kujipatia kipato.

Kabla ya kuanza kilimo cha mahindi lishe, Wema na wanakikundi wenzake, walipewa mafunzo na shirika la Clinton Foundation (CDI Tanzania), kuhusu namna ya kufanikisha kilimo bora cha mahindi lishe.

"Mafunzo hayo yalilenga katika kutujengea uwezo wanakikundi hasa kwa kutuongezea mbinu za kuandaa mashamba, kusimamia na kutumia teknolojia bora na za kisasa za kilimo," anasema Wema

Shirika hilo limewekeza katika kutoa elimu ya kilimo bora, matumizi sahihi ya teknolojia za mbegu, mbolea na masoko ya mazao kwenye wilaya za Kilolo na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

> **Kila ikifika saa nane mchana, ni lazima chakula kiwe tayari mezani ili wanangu wanapofika tu kutoka shule, wafikie kula chakula.**

Wakulima wa mahindi lishe wananufaika na mahindi kwa kuuza mzao yao, pia ni mlo kwao kupikia ugali na uji. Tangu waanze kulima mahindi hayo, sasa kaya nyingi kwenye kijiji cha Malangali zinatumia unga wa mahindi lishe.

"Familia nyingi zimeshazoea kula ugali wa mahindi lishe, ukipika ugali mweupe watoto wanaukataa. Wanapenda sana ugali wa mahindi lishe maana ni mtamu, unaweza kula hata kama hakuna mboga," anasimulia Wema.

### AFYA YAKE

Mahindi lishe yana virutubisho vingi mwilini mwa mwanadamu, ikiongeza Vitamini A inayoimarisha uono wa macho na chakula kitamu kinachopendwa na watu wa rika zote.

"Mahindi lishe yameongeza hata ufaulu wa wanangu shuleni. Kwa mfano mwanangu Eliza wa darasa la saba, ufaulu wake umepanda kutoka kushika nafasi ya 10 mpaka ya tatu mfululizo na amefaulu kwenye mtihani wa taifa," anaeleza mama huyo.

Sasa anasifu kupigana na adui maradhi ujinga, mahindi lishe yakitoa mchango mkubwa kukabiliana na magonjwa mbalimbali, sasa yanatumiwa na wanajamii wengi eneo hilo.Hapo anataja mchango wa kukuza uchumi kwa kuwajengea nguvu wananchi kuwajibikia shughuli zao.

Christian Kufakunoga, ni mume wa Wema anayesema tangu waanze kutumia mahindi lishe wamefanikiwa kuboresha maisha yao na kuondoa udumavu wa akili kwenye familia yao.

"Kabla hatujaanza kula huu ugali familia yangu ilikuwa na shida sana kiafya, lakini kwa sasa imesaidia kuimarisha afya ya familia yangu," anafafanua Kufakunoga

Mume huyo anatafsiri mahindi lishe ni mazao dawa na kwamba watu wanapaswa kuyatumia muda mwingi ili kujenga afya bora. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2020/2021, Wema kwa kushirikiana na wanachama wenzake wa kikundi cha Amani, walifanikiwa kulima ekari 25 za mahindi lishe wakifuata kanuni zote za kilimo bora.

Anafafanua kuwa wamelima ekari hizo wakiwezeshwa na asasi ya Clinton Foundation kupitia CDI Tanzania ikiikopesha kikundi mkopo usio na riba wa pembejeo za kilimo zikiwamo mbegu na mbolea.

Mwanzoni, soko la mahindi lishe lilikuwa chini sana, lakini kwa msaada uliopo kitaasisi anasema wamefanikiwa kupata wateja wa mazao yao kwa bei nzuri. Msimamizi Masoko wa Miradi wa CDI Tanzania, Esther Mhonda, anasema wamejiwekea utaratibu kutafuta wanunuzi mazao yanayozalishwa na wanufaika wao ikiwa ni njia ya kuwahakikishia soko na kuongeza tija.

"Baada ya kuwaunganisha wakulima na soko la uhakika, hali hiyo imeleta ushindani kwa wanunuzi, lakini kukusanya na kuuza mazao kwa pamoja kumefanya bei ya mahindi lishe mwaka huu imekuwa nzuri ukilinganisha na kipindi cha nyuma," anasema Mhonda.

Anaeleza msimu uliopo, kikundi Amani kimejipanga kulima ekari 35, ili kuongeza uzalishaji wa mazao hayo ikilenga faida zaidi na asasi CDI Tanzania imeshasambaza pembejeo kwa wakulima wilaya za Kilolo, Iringa na Mufindi tangu mwishoni mwa mwaka jana, ili kuendana na msimu wa kilimo sasa.

## Ethiopia imeanza kuzalisha umeme Mto Nile baada msuguano miaka 10

**INATOKA UK.13**

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Ethiopia wakati huo, akawaambia wabunge kwamba hakuna nguvu inayoweza kutumika kusitisha ujenzi wa bwawa hilo nchini mwao.

Ilifika hatua Misri, Ethiopia na Sudan zikakubaliana kutumia maji ya Mto Nile kwa pamoja, kuanzia Januari mwaka jana.

Hiyo ni baada ya Mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi hizo tatu huko Washington DC Marekani, katika harakati za kutatua mzozo wa nchi hizo kutokana na bwawa hilo lililozinduliwa wikiendi iliyopita, kuchukua nafasi kuwa kituo kikubwa cha kuzalisha umeme Afrika.

Mkutano huo umekubaliana hakuna upande wowote baina ya nchi hizo utakaosimamisha ujenzi wa mradi huo, Marekani na Benki ya Dunia wakipewa nafadi ya usimamizi wa makubalino ya baadae. Nchi 10 zilizoko katika ukanda wa Bonde la Mto Nile, zina umoja wao ulioanzishwa mwaka 1999 ukiitwa 'Nile Basin Initiative' (NBI) unaoundwa na serikali za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania, Uganda na Eritrea.

Kazi yake kuu ni kusimamia maendeleo endelevu ya ukanda huo kiuchumi na kimazingira, ikiwamo matumizi sawia na sahihi ya maji ya Mto Nile.





## Bil. 7/- kujenga ofisi kuu ya Jiji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetenga Sh. bilioni saba kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kujenga jengo la ofisi kuu ya Jiji inayoendana na hadhi ya makao makuu ya nchi.

Akiwasilisha bajeti ya mwaka 2022/23 kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Jiji hilo, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, alisema kuwa fedha hizo zitajenga ofisi bora na ya kisasa eneo la uwekezaji lililoko Njedengwa na ujenzi wake utaanza Julai mwaka huu.

"Jengo jipya la kisasa la makao makuu ya Jiji litajengwa eneo la Njedengwa ambapo ni katikati ya Jiji kwa hivi sasa kwani jengo linalotumiwa kwa hivi sasa lilijengwa na iliyokuwa ustawishaji wa makao makuu (CDA) mwaka 1973," alisema.

Aidha, Mafuru alisema pamoja na mradi huo, Jiji limeweka kipaumbele kukamilisha miradi yote ya viporo, kuchangia nguvu za wananchi, kujenga ya maendeleo inayoleta tija, kuimarisha seka ya afya, elimu, kilimo na mifugo na utoaji wa huduma katika maeneo ya pembezoni.

Akizungumzia matumizi ya bajeti ya mwaka 2021/22, Mafuru alisema kati ya kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka 2021, Sh. bilioni 13.8 zimetumika katika kutekeleza miradi ya kimkakati, upimaji wa ardhi, malipo ya fidia ya ardhi na miradi ya kijamii.

Pia alisema kujenga Mahakama ya Jiji, ununuzi wa magari matatu kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato na ununuzi wa vifaa vya upimaji ardhi vilivyogharimu Sh. milioni 240, kutoa mikopo kwa vikundi 49 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.04 pamoja na kuendelea kukamilisha mradi wa kimkakati wa hoteli ya Dodoma ya City.

"Pia kuendelea na ujenzi wa miradi ya kimkakati wa kitega uchumi katika mji wa Serikali Mtumba ambacho hadi sasa kimefikia asilimia 90 katika awamu yake ya kwanza," alisema.

Kadhalika, alisema halmashauri imefanikiwa kufanya uthamini wa maeneo mbalimbali ya Nala, Mtumba, Kikombo na Ihumwa ambapo Sh. bilioni 1.32 zimelipwa kama fidia kwa wananchi kupitia mapato ya ndani.

"Katika kipindi hicho Jiji limepima viwanja 10,339 katika maeneo mbalimbali ya Ng'ong'ona, Hombolo Bwawani, Zuzu na Mpunguzi, limeandaa mipango 41 ya matumizi bora ya ardhi," alisema.

# Walimu watakiwa kutoa elimu ya sensa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu, Balozi Mohamed Ali Hamza, amewataka walimu nchini kutumia nafasi zao kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhesabiwa.

Balozi Hamza, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na walimu wa jijini Dodoma kuhusu maandalizi ya sensa ya watu na makazi Agosti mwaka huu.

Alisema walimu wanatakiwa kutumia nafasi zao kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa tukio hilo ili kila mmoja ashiriki.

"Mnatakiwa kushiriki zoezi hili kikamilifu katika pande zote tatu kwanza kuhesabiwa kama raia wa Tanzania, kutoa elimu kupitia nafasi zenu, lakini mkipata nafasi za kuwa wasimamizi au makarani wa sensa," alisisitiza Balozi Hamza.

Aidha, alisema kutokana na jamii kuwasikiliza sana walimu kundi hilo linalowajibu mkubwa wa kuhamasisha watu kujitokeza kuhesabiwa ili serikali iweze kupata takwimu sahihi na kupanda mambo mbalimbali ya maendeleo.

"Mnapaswa kuwatumia wanafunzi kufikisha elimu ya umuhimu wa kuhesabiwa ili na wao wawe mabalozi wazuri katika familia zao ili kufanikishwa kwa asilimia 100 zoezi hili mwaka huu," alisema.

Vile vile, kutokana na umuhimu wa sensa ya watu na makazi, aliwataka walimu kuendelea kuikumbusha jamii kila wakati na asitokee mtu hata mmoja ambaye atakwenda kinyume na malengo ya serikali.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema zoezi la sensa ni la kitaifa na kimataifa ambalo linasaidia kujibu kila kitu kinachoihusu nchi husika.

Dk. Chuwa alisema sensa ya mwaka huu ni tofauti na zile zote ambazo zimewahi kufanyika nchini.

"Sensa ya mwaka huu itakuwa ya kisasa sana hatutatumia tena makaratasi, lakini tunakwenda kuhesabu kila jengo lililoko nchini iwe hospitali, kiwanda, godauni ili kupa kila kitu na kujua kipo wapi," alisema Dk. Chuwa.

Pia alisema zoezi la sensa mwaka huu watatumia mipaka ya vitongoji kuhesabu watu na teknolojia watakayotumia ni vishikwambi.

"Baada ya kumalizika kwa tukio hili la sensa ya watu na makazi vishikwambi vyote tunakwenda kuvikabidhi kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ili wavitumie kusahihishia mitihani yao," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema kutokana na umuhimu wa sensa ya watu na makazi mkoa umeona ni vyema kuwakutanisha walimu na viongozi wanaoratibu zoezi hilo.

"Walimu ni jeshi kubwa ambalo litatusaidia kufanikisha zoezi hili la sensa mwaka huu hivyo tumeona ni muhimu wakakutana na wataalamu kutoka ofisi ya taifa ya takwimu ili kupata elimu na kuuliza maswali yao ili kuongeza ufanisi wakati wa kutekeleza zoezi hili," alisema Mtaka.



Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Zainabu Chaula (kulia), akimsikiliza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, walipokutana kwenye mkutano wa viongozi wa wamachinga nchini, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Haki za wanafunzi wenye mahitaji maalum zitambuliwe'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Elimu Maalum Jiji la Dodoma, Issa Kambi, ameitaka jamii kutambua haki za kimsingi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili wafikie ndoto zao kielimu.

Kambi aliyabainisha hayo alipokuwa akizungumza na wadau mbalimbali wa elimu kwenye kikao cha kujadili jinsi ya kuwapatia mahitaji wanafunzi wenye ulemavu kilichofanyika jijini hapa.

Ofisa huyo alisema watoto wenye ulemavu wanaendelea kufanyiwa ukatili wa kufungiwa ndani na kukosa fursa mbalimbali ikiwamo elimu.

Alisema jamii inapaswa kutambua umuhimu wa kuwasaidia wanafunzi hao misaada mbalimbali, ili kukabiliana na vikwazo vinavyowakabili.

"Kuna mifano iliyo hai mimi kama ofisa elimu, elimu maalum ambayo imeshuhudia kwa kuona, baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto ambao wana ulemavu wamekuwa wakiwaficha watoto hao majumbani, wakati watoto hao wana vipaji ambavyo wanaweza kufanya na wakaweza kujikimu kimaisha," alibainisha.

Naye mmoja wa wadau wa elimu, Mchungaji Emmanuel Andrew wa Kanisa la SDA, alisema "Changamoto kubwa iliyoko hapa bado kuna wazazi ambao wanawaficha watoto majumbani na kuwakosesha haki zao za kimsingi ikiwamo elimu, matibabu na hata na kulindwa, kwa hali hiyo ndiyo maana mahitaji yao yanalindwa na kusaidiwa kwa usahihi."

Naye Pendo Maiseli kutoka Taasisi isiyo ya kiserikali ya Action for Community Care (ACC) Dodoma, aliomba idara ya elimu maalum ya jiji hilo kutoa takwimu sahihi za wanafunzi wenye ulemavu ili kufikiwa na kupatiwa misaada inayohitajika.

Maiseli alisema kuwa tatizo lililoko kuzipata takwimu sahihi kwa wataalamu wa elimu maalum.

"Hili ni tatizo ndio maana wanafunzi walio wengi baadhi yao wameshindwa kufikia malengo yao kutokana na kukosa mahitaji yao malum ambayo yangeweza kuwasaidia," alisema.

Kwa upande wake, Justire Mbasha kutoka Shirika lisilo la kiserikali la Afnet Dodoma, alisema kuwa pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na mashirika na taasisi mbalimbali yasiyo ya kiserikali, bado wazazi na walezi hawatoi ushirikiano wa uwapo wa watoto wenye ulemavu ndani ya familia zao.



# Wakulima waiangukia serikali mgogoro ardhi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAKULIMA wa Kijiji cha Ikama Kata ya Itagata katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro unaofukuta baina yao na Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa kuwa unatishia amani kwenye eneo hilo.

Wananchi hao wanadai bodi hiyo imewapora mashamba yao yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 140 kwa maelezo kuwa yako kwenye chanzo cha maji cha Mto Mbaka na hivyo hawatakiwi kuendelea kufanya shughuli za kilimo.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wananchi hao walidai maofisa wa bonde hilo waliingia kwenye mashamba yao na kuanza kuweka alama za mipaka bila kuwashirikisha chochote, hivyo kuzua taharuki miongoni mwao.

Mmoja wa wananchi hao, Karim Katwange, alidai kuwa mashamba yao yalizungushiwa mipaka bila wao wenyewe kuwa na taarifa na walipoziona waliamua kuwauliza viongozi wao wa kijiji na kata ambao pia walidai kutokuwa na taarifa.

Alisema kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakilima mashamba hayo kwa kufuata sheria za utunzaji wa vyanzo vya maji na hivyo kitendo kilichofanywa na maofisa hao kutaka kuwazuia kulima mashamba yao ni kinyume cha sheria.

"Mimi binafsi wamechukua ekari saba ambazo baadhi nimepanda migomba, mahindi, miche ya maparachichi na mengine yana chai, walikuja kuweka hizi alama bila kutushirikisha, sasa ingetokea tukaamua kuwadhuru si zingetokea vurugu?" Katwange alihoji. Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikama, Julius Mwatebela, alisema viongozi na wananchi hawakushirikishwa wakati wa kuweka alama hizo na walibaini ni maofisa wa Bonde la Ziwa Nyasa kutokana na maandishi yaliyoko kwenye alama hizo.

Alisema kuwa katika mashamba hayo wananchi wamepanda mazao mbalimbali yakiwamo ya biashara, chakula pamoja na miti ya mbao ambayo baadhi imefikia umri wa kuanza kuvunwa.

Alisema moja kati ya mashamba yaliyozungushiwa alama ni shamba la kijiji ambalo lina chai iliyopandwa mwaka 1970 na shamba hilo mpaka sasa linamilikiwa na kijiji hicho.

"Sisi hatukushirikishwa chochote na ndiyo maana tumeshtuka, mashamba haya tumekuwa tukilima kwa kufuata taratibu za utunzaji wa mazingira na ndiyo maana hatujagusa kwenye kingo za mto," alisema Mwatebela.

Kaimu Meneja wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa, John Kavishe, alikiri taasisi hiyo kuweka alama hizo na kufafanua kuwa wanachokifanya ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kutunza vyanzo vya maji.

Vilevile, alisema ofisi yao ilitembelewa na Mkuu wa Wilaya hiyo ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, Desemba 16, mwaka jana, ambaye aliwaagiza kukitunza chanzo hicho cha maji cha Mto Mbaka.

Alisema eneo walilozungushia lina ukubwa wa hekta 57.2 na kwamba eneo hilo linahifadhiwa kwa sababu ni eneo oevu na hivyo lazima lihifadhiwe lote badala ya chanzo cha maji pekee.

"Zoezi linaendelea la utunzaji wa chanzo kile, baada ya kuweka zile 'bicorn' (alama) kinachofuata ni utoaji wa elimu kwa wananchi na tuliamua kuweka kwanza alama kwa sababu tulikuwa tunakimbizana na msimu wa kilimo," alisema Kavishe.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa sheria, hakutakuwa na fidia yoyote kwa wananchi hao kwa maelezo kuwa wao ndio waliovamia chanzo cha maji.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Anney, alisema ofisi yake inashirikiana na Ofisi ya Bonde kuyabainisha maeneo hayo ambayo yanatakiwa kuhifadhiwa na kinachofuata ni elimu kwa wananchi.



Wakazi wa Kijiji cha Ikama, Kata ya Itagata, wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wakionyesha baadhi ya alama zinazodaiwa kuwekwa kwenye mashamba yao na maofisa wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa, ili kuwazuia kulima mashamba hayo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TASAC yapigia debe usafirishaji kwa meli

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SHIRIKA la Uwakala wa Meli (TASAC) limewataka wananchi kusafirisha mizigo kwa njia ya maji kwa kuwa njia hiyo ni rahisi zaidi na ni nafuu kuliko njia zingine.

Meneja wa Udhibiti Huduma za Usafiri kwa Njia ya Maji, Fatma Masenene, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati maofisa wa TASAC kutoka makao makuu walipotoa elimu kwa wadau wa usafirishaji jijini.

Alisema usafiri wa njia ya maji ni rahisi kwa kuwa unasafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja na kwa bei nafuu kuliko wanaotumia njia ya barabara na zingine.

Alisema kwa mujibu wa sheria, TASAC ndiyo chombo ambacho kimepewa mamlaka ya kuwasajili wasafirishaji wa mizigo kwa njia ya maji na ndiyo sababu ya kuamua kushirikiana na wadau wengine.

"Tunashirikiana na Bodi ya Wasafirishaji Tanzania na kwa bahati mbaya huku Mbeya hakuna wale mawakala wa usafirishaji wa mizigo midogo, sasa tumekuja huku kuhamasisha wananchi kusafirisha mizigo kwa njia ya maji kwa sababu ni njia rahisi na nafuu zaidi," alisema Fatma.

Alisema usafirishaji wa mizigo kwa njia ya maji unasaidia kuokoa barabara zisiharibike haraka na hivyo kukaa muda mrefu bila kuharibika na kupunguzia serikali gharama za matengenezo ya barabara.

Baadhi ya wadau wa usafirishaji waliishukuru TASAC kwa kutoa elimu hiyo wakidai kuwa baadhi ya vitu walikuwa hawajui na walikuwa wakiamini kuwa huduma hiyo ni kwa wasafirishaji wa mizigo mkubwa pekee.

# Mkandarasi kitanzini kuchelewesha mradi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

UONGOZI wa Mkoa wa Mbeya umetishia kumchukulia hatua za kisheria mkandarasi anayejenga daraja la Mto Mbaka wilayani Rungwe kutokana na kuchukua muda mrefu bila kukamilika huku wananchi wakipata shida ya usafiri.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa angalizo hilo juzi wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipozuru kukagua ujenzi wa daraja hilo ambalo limejengwa kwa muda mrefu bila kukamilika licha ya mkandarasi kulipwa fedha zote.

Homera alimtaka mkandarasi huyo, Kampuni ya Summer Communication LTD kukamilisha mradi huo ndani ya miezi miwili na endapo hatakamilisha, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Alisema baada ya miezi miwili kupita kamati hiyo itafanya tena ziara katika eneo hilo kwa ajili ya kuangalia kama daraja hilo litakuwa limekamilika na kwamba ndipo hatua zitakapoanza kuchukuliwa kama litakuwa halijakamilika.

Alisema kitendo cha makandarasi wazawa kuchelewesha miradi kinasababisha kutoaminika na hivyo kutopatiwa zabuni kwenye miradi ya serikali.

"Usipokamilisha tutamwagiza Meneja wa TARURA kuvunja mkataba na tutapelekana mahakamani, lakini mnajiharibia kazi wenyewe maana kuna mwingine kule Chunya naye ni mzawa kama wewe, naye anachelewesha mradi," alionya.

Homera alisema kipaumbele cha serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri lakini inapotokea mkandarasi anachelewesha mradi, anasababisha wananchi kuichukia serikali.

Alisema kwa sasa TARURA wana fedha za kutosha na makandarasi wanaofanya kazi vizuri ndiyo watakaokuwa wanapata zabuni na wale ambao sio waaminifu wataendelea kukosa kazi.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo walisema kutokana na kuchelewa kukamilika kwa daraja hilo, wamekuwa wakipata shida ya usafiri kutokana na daraja la zamani kutokuwa imara.

Mmoja wa wananchi hao, Huruma Mwakalonge, alisema wananchi wa maeneo hayo wanakwenda kutibiwa katika Hospitali ya Ntaba, lakini kutokana na kutokamilika kwa daraja hilo wanatumia muda mwingi kuzunguka kwenda kuvuka kwenye eneo lenye daraja ambako ni mbali. Vilevile, alisema daraja hilo ndilo wanalolitegemea kuvusha mazao yao kwenda kwenye masoko, hivyo mkandarasi huyo anawachelewesha kuinuka kiuchumi.

"Hapa kama mnavyoona magari makubwa hayawezi kuvuka kiurahisi, sasa tunamshukuru Mkuu wa Mkoa ameamua kuja kutembelea daraja hili na kutoa hamasa, tunaamini itasaidia kuongeza kasi," alisema.

Tegemea Baraza, mkazi wa Kijiji cha Kisegese, alisema ubovu wa daraja lililoko unawatesa zaidi wajawazito ambao hulazimika kusafirishwa kwa bodaboda kwenda kujifungua.



# Waziri ataja sababu kuchelewa malipo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhammed Said, amekiri kuwa baadhi ya walimu huchelewa kupata posho za usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya taifa kutokana na sababu mbalimbali.

Amesema moja ya sababu za kuchelewa huko ni kuwasilisha taarifa za kibenki au kuwasilisha taarifa zisizo sahihi.

Simai aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kwahani, Yahya Rashid Abdulla, aliyetaka kujua sababu zinazofanya walimu kuchelewa kupata malipo yao wanapomaliza kazi.

Alisema baadhi ya walimu wa jinsi ya kike huwasilisha akaunti za waume zao licha ya kuwa wao ndio waliofanya kazi na wanaostahiki kupokea malipo badala ya waume zao. Waziri Simai alitaja sababu zingine ni kuchelewa kupatikana kwa fedha iliyoombwa kutoka serikalini. Alisema hali hiyo ilijitokeza katika mwaka wa fedha 2020/21 kulikosababishwa na janga la UVIKO- 19.

"Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha mjumbe kuwa hakuna tofauti ya malipo kwa kazi ya usahihishaji wa mitihani baina ya walimu walioko Pemba na wale walioko Unguja. Walimu hawa hulipwa posho kwa kutegemea kazi wanayoifanya, dhamana aliyokabidhiwa na idadi ya siku aliyofanya kazi," alisema.

Pia alisema utaratibu wa kulipwa posho kwa walimu wanaoshiriki katika kazi maalumu ya usimamizi na usahihishaji wa mitihani taifa kwa Unguja na Pemba ni wa aina moja.

Waziri huyo alisema kazi ya usahihishaji wa mitihani ya taifa hufanyika katika vituo maalumu vilivyoteuliwa kwa kuwa na mazingira yanayoridhisha na baraza linahakikisha kuwa kila mwalimu anapatiwa mahali pa kulala.

Alisema hakuna uhaba wa vifaa kama magodoro katika vituo vya usahihishaji wa mitihani ya taifa kwa kuwa maandalizi ya vituo hufanyika mapema ili kuondosha changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza ikiwamo kuazima magodoro ya ziada pale yanapohitajika kutoka katika taasisi nyingine ya serikali.

## Chanzo cha kusuasua ujenzi chabainishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUCHELEWA kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) Chakechake Kisiwani Pemba kunatokana na shirika hilo kukosa fedha za kumlipa mkandarasi ili kuendelea na kazi ya ujenzi, imeelezwa.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chakechake, Shaib Hassan Kaduara, aliyetaka kujua sababu zilizofanya jengo hilo kutokujengwa.

Alisema fedha ambazo shirika hilo lilikuwa linakusanya kwa kipindi hicho cha Julai – Oktoba zilikuwa zikitumika kwa ununuzi wa karafuu.

Kwa mujibu wa waziri, mwaka 2021/22 ulikuwa msimu mkubwa wa mavuno ya karafuu, hivyo shirika lililazimika kutumia fedha nyingi kwenye ununuzi ili kuwahudumia wakulima wa karafuu.

Aidha, alisema kwa sasa ujenzi wa jengo hilo unaendelea na kwamba Januari 3, mwaka huu, mkandarasi alirejea katika eneo la ujenzi kwa kuendelea na kazi.

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chakechake, Shaib Hassan Kaduara, aliyetaka kujua sababu zilizofanya jengo hilo kutokujengwa.**



Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Zantel, Moses Alphonce, akizungumza wakati wa semina ya uboreshwaji wa huduma ya Ezypesa, iliyoandaliwa na kampuni hiyo inayojulikana Ezypesa Forums 2022, iliyofanyika Kiembesamaki, mjini Zanzibar juzi. Kushoto kwake ni Anne Killindu na (kulia kwake), Suleiman Salum Abdalla ambao ni maofisa wa Ezypesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Maduka mapya ya fedha yaibua fursa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim, amesema kuondolewa kwa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni ambayo si rasmi kumesababisha kuongezeka kwa benki 13 za biashara ambazo zimekuwa zikitoa huduma hizo.Benki hizo, amesema ambazo zina matawi sehemu mbalimbali za mji, sambamba na maduka matatu ya Posta.

Waziri huyo aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Shaurimoyo, Hamza Hassan Juma, aliyehoji kwamba kuondoa maduka hayo kumesababisha usumbufu mkubwa kwa wageni wanaofika Zanzibar.

Alisema mwaka 2018 serikali ilifanya ukaguzi maalum wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini baada ya kuwapo kwa taarifa ya kukithiri kwa ukiukwaji wa sheria na kanuni, ikiwamo ukwepaji kodi.

Pia alisema maduka hayo yalisababisha wamiliki kutokutoa risiti kwa miamala inayofanyika, kuwasilisha taarifa zisizo sahihi na kutodai utambulisho wa wateja wanaobadilisha fedha za kigeni.

Alisema katika ukaguzi huo, maduka mengi ya kubadilisha fedha za kigeni yalifungwa baada ya kuthibitika kuwa yalikuwa yanaendesha biashara kinyume cha sheria za nchi.

Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania, alisema tayari imeshatoa leseni kwa kampuni ya Furaha Safari Ltd ya kuanzisha duka jipya la kubadili fedha za kigeni Zanzibar, ambalo litaongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

"Sambamba na hayo, fursa ziko wazi kwa wale wote wanaotaka kuendelea na huduma pindi wakikidhi vigezo vilivyowekwa," alisema Waziri Jamal.

Pia alisema serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilitoa mwongozo kwa maduka yote yaliyofungiwa kufata utaratibu uliowekwa kwa kuzingatia sheria na kanuni za nchi.

Hata hivyo, alisema wananchi wanaotaka kuendelea na biashara ya kubadilisha fedha za kigeni wanatakiwa kufata masharti na vigezo vilivyowekwa kisheria.

"Kwa kufanya hivyo, vijana wetu wengi ajira zao zitarudi na wataendelea na shughuli zao za biashara na uchumi na hatimaye kupunguza umaskini," alisema.

Waziri alisema jitihada za serikali zinaendelea katika kuimarisha sekta ya fedha nchini na sekta zingine kwa lengo la kuinua vipaji na kutoa fursa kwa vijana wa taifa la kesho.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**
**BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA JIJI**

SIMU:MKURUGENZI :
OFISI ZOTE :255 -28- 40334
FAX:255 028 2500785
E-mail: mwanzacity@thenet.co.tz

IDARA YA MIPANGO MIJI
MAZINGIRA NA UTALII
KITENGO CHA ARDHI
S.L.P 1333
MWANZA
6.1.2022

Kumb Na: MCC/L/19783/8/CDM

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA.

**YAH: UPOTEVU WA BARUA YA TOLEO "OFFER "KIWANJA NAMBA 51 KITALU "BIX" MKUYUNI WILAYA YA NYAMAGANA –JIJI LA MWANZA.**

**Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.**
Ofisi imepokea taarifa ya upotevu wa barua ya toleo **"Letter of Offer" Kutoka kwa PAUL LEO wa S.L.P 1700 MWANZA** ambae ni mmiliki wa kiwanja tajwa hapo juu.

Hata hivyo tumeshindwa kuendelea na utaratibu wa kawaida wa kumwandalia hati ya umiliki wa kiwanja hicho kutokana na kukosa barua hiyo ya toleo kama ilivyoelezwa hapo juu.

Kabla ya kuchukua hatua nyingine za kisheria, ofisi yetu inatoa tangazo kwa yeyote mwenye barua hiyo ya toleo au kujua ukweli tofauti aijulishe ofisi yetu kwa mawasiliano tajwa hapo juu au kuipeleka katika kituo chochote cha polisi ndani ya siku thelathini (30) tangu tarehe ya barua hii.

Halima I.N
Kny: MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Gregory Gad Magambo** anatangaza kupotea kwa Kadi ya Pikipiki yenye namba za Usajili **MC. 471 BAV.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichopo jirani yake, Taarifa ya Polisi .

**MBE/RUJ/RB/74386/2022.**

## MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu (Home chattels) katika yard ya Makumbusho. Mnada utaendeshwa na dalali tajwa hapo chini kwa idhini waliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kwa majina yaliyotangazwa gazetini:-

1. Rehema Leonardy Sekele
2. Hadija Mustapha Habibu
3. Asha Seleman Mohamed
4. Joyce Method Rwegasira
5. Esther Emmanuel Mayunga
6. Abuubakary Tamimu Jumbe
7. Rehema Saidi Pazi
8. Shina Rehege
9. Sabina Simon Kusaduka
10. Rukia Salum Rajabu
11.Regina John Hiluka

Mnada utafanyika tarehe 10/03/2022 mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za ubebaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**WHITE MIRACLES (T)LIMITED :0684937219**
**GSP Auction Mart: 0719744248**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SELEMAN KHATIB FAKHI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota PREMIO yenye namba za usajili T 816 BMT. Chassis No. AT2110067410, Engine No.7AG911037. yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi DOD/-DOD/RB/77236/2022.

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MWANZA AT MWANZA**

**RM MISC CIVIL NO.48 OF 2021**

**FADHILI YOHANA MBELWA & 2 OTHERS ........PLAINTFF**
**VS**
**IMANI VEDASTO SIRIKIAKUSI & 2 OTHERS.....................................................DEFENDANT**

**TO; JULIUS MASIRORI MAHERI**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for mention/hearing on 16 day of 03, 2022 at 8:30a.m.

YOU ARE hereby required to appear in this court without fail and you must produce on that day all documents required.

Given under my Hand and Seal of the Court this 16 day of 02, 2022.

.................................
**SENIOR RESIDENT MAGISTRATE**
**MWANZA.**

TO BE SERVED UPON.

## TANGAZO KWA UMMA.

Kampuni ya **PMM ESTATES (2001)** itasafirisha mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Rufiji kwenye mradi wa bwawa la kufua umeme.

Vipimo ni **17.5m urefu, 3.2m upana, na 4.8m kimo**

Baadhi ya gari zitakazotumika ni **T591DVW/T159DUL, T579DVW/T101DUL, T595DVW/T155DUL, T637DVW/T171DUL, T598DVW/T162DUL, T790DVW/T174DUL, T614DVW/T990DUK, T799DVW/T164DUK, T692DVW/T163DUL, T797DVW/T172DUL, T864CVX/T472CVG, T904CVX/T473CVG**

Safari imepangwa kuanza tarehe **23.02.2022**

Njia zitakazotumika ni barabara ya ***Mandela na ya Kilwa hadi Kibiti na kwenda Mloka hadi kwenye mradi.***

Muda wa safari ni kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

116720702

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RC aridhishwa ABSA utunzaji wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, ameipongeza Benki ya Absa kwa mchango mkubwa inaotoa katika kuboresha mazingira nchini.

Kagaigai alitoa pongezi hizo wakati akipokea miche 2,100 ya miti ya asili kutoka kwa uongozi wa benki hiyo, katika ofisi za Mkuu wa Mkoa, zilizoko Moshi.

"Kumekuwapo juhudi kubwa zinazolenga kuboresha mazingira mkoani hapa, niwapongeze kwa mchango wenu huu muhimu na pia nitoe rai kwa taasisi zingine kuiga mfano wenu," alisema.

Aidha, aliupongeza uongozi wa Benki ya Absa kwa kutoa miche ya miti ya asili ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa utunzaji wa vyanzo vya maji.

"Mkoa huu ndiyo nyumbani kwa Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote barani Afrika, kuendelea kuweko kwake mlima huu ni vyanzo vya maji vihifadhiwe, hivyo miche ya miti ya asili itachangia katika utunzaji wa vyanzo hivyo muhimu," alisema.

"Mlima Kilimanjaro ndiyo chanzo cha maji ambayo yanatumika kwa masuala mbalimbali ya kiuchumi kama vile uvuvi, kilimo, mazingira bora na matumizi aina mbalimbali kwa shughuli zinazofanywa na binadamu, hivyo miti ya asili ni muhimu ili vyanzo vizidi kuhifadhiwa," alisema.

Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Benki ya ABSA, Aron Luhanga, alisema miche hiyo ni sehemu ya mchango wa benki hiyo kwa jamii kupitia mashindano ya Kilimanjaro Marathon ambayo Benki ya Absa inadhamini kwa mwaka wa tatu sasa.

# Elimu chanjo ya UVIKO-19 yahitajika kufuta dhana potofu

**Na Mary Geofrey**

MABARAZA ya Wataalamu wa Afya, yametakiwa kutekeleza vyema jukumu la kuelimisha na kuhamasisha watoa huduma za afya kuchanja chanjo ya UVIKO-19 kwa kuzingatia kuwa jamii inawategemea wao.

Aidha, watoa huduma za afya wametakiwa kutumia nafasi zao za kuaminika ndani ya jamii, kutoa elimu na kuwabadili wananchi kuhusu dhana potofu ya chanjo ya UVIKO-19.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS), Prof. Deudatus Kakoko, aliyasema hayo juzi, kwenye mkutano kwa njia ya mtandao wa Zoom na wasajili wa bodi za kitaalamu za afya kwa lengo la kuweka mikakati ya kuongeza kasi ya uchanjaji wa chanjo ya UVIKO-19.

"Wataalamu wa afya wanaaminika zaidi kwenye jamii zetu, jamii inaamini hawa ndio madaktari sahihi na ndio wanaofahamu chochote kuhusu afya, hivyo ni muhimu wakatumia fursa hii adhimu kuielimisha jamii kuhusu chanjo ya UVIKO-19.

"Wananchi wana imani potofu kuhusu chanjo, Mabaraza ya Afya hili ni jukumu lao kuisemea serikali, kuwaondoa hofu wananchi kisayansi na kitaalamu kuhusu faida na umuhimu wa chanjo hizi," alisisitiza Prof. Kakoko.

Aliendelea kusema kuwa, inahitajika mikakati thabiti ya namna ya kuondokana na imani potofu kwa kutumia taarifa za kitafiti na za kitabibu ili kutoa taarifa sahihi.

"Hii itasaidia kuielimisha jamii na hivyo kuondokana na imani potofu. Ni muhimu kuendelea kutoa elimu katika makundi yote ya jamii wakiwamo wataalamu wa afya ili kuepusha ombwe la taarifa juu ya chanjo ya UVIKO-19 na kuwafanya wawe mstari wa mbele kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19," alihimiza Prof. Kakoko.

Aidha, alisema mamlaka husika iendelee kusisitiza na kuielimisha jamii juu ya sheria za mitandao ili watu waepuke kusambaza taarifa potofu.

Alitaja sababu ya imani potofu kuongezeka ni baadhi ya makundi kuwa katika hatari au kuwa na uwezekano wa kuathirika zaidi wakati hakuna utafiti unaoonyesha kuwa UVIKO-19 ni ugonjwa wa makundi mahususi.

"Ukweli ni kuwa UVIKO-19 hauna mipaka kwa wazee, matajiri wala mjini hivyo chanjo zinahusu makundi yote ya jamii. Takwimu zinaonyesha tatizo la UVIKO-19 bado lipo na kuna uwezekano wa tatizo kuongezeka," alisisitiza.




Mkazi wa Dar es Salaam, akiangalia kilainishi kinachotengenezwa na kampuni ya mafuta ya Puma Energy, alipotembelea maonyesho ya Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania, jijini humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sekta ya Uvuvi kuipaisha Singida kimapato

**Na Elisante John,** SINGIDA

MANISPAA ya Singida imeanza kuimarisha vyanzo vyake vya mapato vya ndani, ikiwamo sekta ya uvuvi katika mabwawa makubwa mawili, maarufu Ziwa 'Singidani na Kindai', yaliyoko pembezoni mwa mji wa Singida.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alisema jana kuwa ili sekta hiyo ichangie kikamilifu pato la ndani, shughuli za uvuvi ndani ya Ziwa Kindai na Singidani kwa muda wa miezi mitano zitasitishwa ili kupisha samaki kuzaliana na wavuzi kukata leseni mpya.

Alisema ili kudhibiti shughuli za uvuvi, wameanza msako na tayari wamekamata wavuvi kadhaa na nyavu, huku akiahidi jambo hilo lililoanza Januari 31, hadi Mei 31, mwaka huu, litakuwa endelevu.

Katika msako huo unaojumuisha maofisa wa idara za uvuvi, biashara na askari mgambo, Nipashe ilishuhuda nyavu nne kubwa na mitumbwi miwili ikiwa imekamatwa baada ya kutelekezwa na wavuvi wanaokaidi zuio hilo.

"Maziwa haya mawili yana mchango mkubwa kwa uchumi wa mji wetu. Hatuwezi kuyaacha hivi hivi kipindi hiki. Sasa samaki wakubwa wanaoishi kwenye kina kirefu wanalazimika kuja juu kutafuta matingatinga katika kina kifupi ili kutaga mayai," alisema.

Katika kuhakikisha manispaa inafanikisha zuio hilo, alisema wanatarajia kupokea boti moja kutoka bonde la kati la maji, itakayotumika mchana na usiku hasa katika Ziwa Kindai ili kudhibiti wavuvi wasiotaka kutii taratibu na sheria.

Aidha, Lupembe alifafanua kuwa, tayari kikosi kazi maalum kimeundwa kwa ajili ya kufanya msako wakati wowote mchana na usiku, ili wale wote watakaoshindwa kutii zuio hilo, wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Alibainisha kipindi hiki ambacho ziwa limefungwa, wavuvi watumie nafasi hii kwenda kukata leseni ya uvuvi, kwa ajili ya kurahisisha shughuli za uvuvi na kulipa kodi kwa mujibu wa sheria za nchi.

Ofisa Mifugo na Uvuvi Manispaa ya Singida, Dk. Adrianus Kalekezi, alisema Ziwa Singida na Kindai yana wavuvi 150 wanaoweza kuongeza mapato ya ndani, kutokana na malipo ya ushuru na kodi, pia kwa leseni mpya watakazokata.

Dk. Kalekezi alisema maziwa hayo yenye samaki aina ya perege na furu, yana idadi hiyo ya wavuvi ambao kati ya Juni hadi Desemba, mwaka jana, waliingizia manispaa mapato ya Sh. milioni 280 kutokana na tani 35 za samaki.

Mmoja wa wavuvi, Salum Kikokomeko, anayevua samaki katika maziwa hayo kwa muda mrefu sasa, alisema kuyafunga maziwa hayo ni kuwasumbua wavuvi kwa kuwa wengi wao ni wa kipato cha chini kutokana na zana duni wanazotumia wakati samaki walioko ni wengi.

Kutokana na hali hiyo, Kikokomeko alitumia fursa hiyo kuiomba Manispaa ya Singida, kukutana na wavuvi mara kwa mara, ili kubadilishana mawazo yenye nia ya kuleta tija baina ya pande zote.

HABARI MICHEZO

# KOCHA SIMBA KUVAA VIATU VYA MAKATA DODOMA JIJI

Na Saada Akida

UONGOZI wa Klabu ya Dodoma Jiji, umesema upo kwenye mazungumzo na aliyekuwa Kocha Msaidizi wa Simba, Mrundi Masoud Djuma, ili kuja kukinoa kikosi cha timu hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Dodoma Jiji FC, Fortunatus Johnson, alisema wanafanya mazungumzo na kocha huyo lakini bado hawajafikia muafaka.

**Alisema wanaendelea na mchakato huo baada ya kufanya mazungumzo ya awali, na wanaamini kama yakienda vizuri, atakuja nchini kwa ajili ya kuinoa timu hiyo.**

"Tunafanya mazungumzo na kocha huyo [Masoud], bado hatujakubaliana chochote na mambo yakienda vizuri tutaweka wazi kama tutafanikiwa kuafikiana," alisema Fortunatus.

Alisema maboresho hayo wanayotaka kuyafanya katika benchi la ufundi ili kuhakikisha timu yao inafanya vizuri na kupata matokeo mazuri kwenye michezo iliyoko mbele yao ya Ligi Kuu.

Kuhusu Kocha Mkuu, Mbwana Makata, katibu huyo alisema bodi itakutana kwa ajili kujadili mwenendo wa timu hiyo pamoja na mchakato wa kocha mpya ikiwamo nafasi ya Makata ndani ya timu hiyo.

Hata hivyo, taarifa nyuma ya pazia zilizolifikia gazeti hili kutoka kwa vyanzo vyake zimeeleza kuwa tayari Masoud amemalizana na uongozi wa Dodoma Jiji FC na wakati wowote anaweza kutua nchini kwa ajili ya kusaini mkataba wa kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Dodoma Jiji ipo katika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 17 baada ya kushuka dimbani mara 15 na kushinda michezo minne, sare tano na kupoteza sita.

TUNAELEWANA?...



Mratibu wa Kituo cha Mkono kwa Mkono (One Stop Centre), kinachohudumia manusura wa vitendo vya ukatili, Asia Mkini, akizungumza na wachezaji wa timu ya soka ya Morning Star jana jijini Dar es Salaam, katika mwendelezo wa utambulisho wa mradi wa majaribio unaolenga kukabiliana na vitendo hivyo katika jamii, ambao unaendeshwa na LHRC kwa kushirikiana na JICA. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Coastal Union kujadili mrithi wa kocha Medo, Zahera atajwa

Na Saada Akida

JOPO la uongozi wa Klabu ya Coastal Union linatarajiwa kukutana mwishoni mwa wiki hii, kuzungumzia mwenendo wa timu yao na kutangaza kocha mpya atakayekinoa kikosi cha timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hatua hiyo imekuja baada ya Coastal Union kupoteza mechi tano mfululizo za ligi hiyo zilizoandamana na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mmarekani Melis Medo kujiuzulu na kutimkia Dar es Salaam kwa mapumziko mafupi.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka ndani ya uongozi wa klabu hiyo, zimeeleza kuwa mwenendo wa matokeo mabaya wa timu hiyo, ndio uliomfanya Melis kujiuzulu na kuondoka jijini Tanga.

Chanzo chetu hicho cha uhakika kilieleza mwishoni mwa wiki hii kwamba watakutana kujadili mwenendo wa timu na kwamba tayari wamebaini kuna baadhi ya watu waliokuwa wakimfanyia hujuma kocha huyo, ambao watachukuliwa hatua kali na kuna uwezekano mkubwa Mwinyi Zahera kuchuwa nafasi ya Melis.

"Ni kweli kocha Melis hana furaha kabisa na matokeo ya mechi tano tulizopoteza za Ligi Kuu, ukizingatia timu inacheza vizuri na kama kuna watu wanaihujumu, tutajua baada ya kikao hicho," alisema na kuongeza.

"Ikigundulika kama kuna watu kweli walikuwa wanamhujumu kocha huyo, watachukuwa maamuzi magumu iwe ndani ya uongozi au benchi hilo la ufundi," kilisema chanzo hicho huku kikiomba hifadhi ya jina lake.

Kocha Melis Juzi hakuwapo mazoezini na kikosi kikiwa chini ya Kocha Joseph Lazaro aliyesimamishwa kipindi cha nyuma kwa kushindwa kuelewana na kocha huyo raia wa Marekani.

Mbali na Lazaro, pia wachezaji wa zamani wa Coastal Union walifika mazoezini kwa ajili ya kuzungumza na wachezaji kuhusu mwenendo mbaya wa timu hiyo kwenye ligi.

Melis ameondoka Coastal Union akiiacha katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 17 baada ya kushuka dimbani mara 15 na kushinda michezo minne, sare tano na kupoteza sita.

## Vivier ataja Biashara ilipoishika Azam FC

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Biashara United, Vivier Bahati ametoa siri ya kuifunga timu ya Azam FC mabao 2-0 katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC waliocheza juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza huku akitaja neno "kuifahamu" kumemsaidia.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo Vivier ambaye awali alikuwa kocha msaidizi wa Azam FC kabla ya kutua Biashara United, alisema wamepata ushindi huo kiurahisi kwa kuwa anaifahamu vizuri timu hiyo yenye maskani yake Chamazi, Dar es Salaam.

"Azam wanashambulia kwa kuanzia nyuma, hivyo ukiwaacha mabeki wao na viungo wawe huru na mpira miguuni ni hatari lakini ukiwaachia mabeki wao na viungo wawe huru na mpira ni hatari.

"Nilichofanya ni kutumia mfumo wa kukabia juu, kwa kuanzia kwenye goli lao, hii ilitusaidia kwani hawakuwa huru kufanya mashambulizi waliyozoea. Wachezaji wangu wakaweza kufuata maelekezo niliyowapa na tukafanikiwa kupata pointi tatu," alisema Vivier.

Alisema anawashukuru wachezaji kwa kupambana na kufanikiwa kupata pointi tatu kwenye mchezo huo ambao ulikuwa na ushindani mkali, lakini akiwashukuru mashabiki wao kutokana na ushirikiano wanaouonyesha.

"Nawapongeza wachezaji kwa kazi kubwa waliyoifanya mpaka tukafanikiwa kupata ushindi mzito kama huu," alisema.

Aidha, Vivier alisema kama wangekuwa makini wangetoka na idadi kubwa ya mabao, lakini ameridhika kwa sababu haiwezekani kila nafasi kuitumia kufunga.

Kwa matokeo hayo, hiyo inakuwa mechi ya kwanza Ligi Kuu kwa Kocha Mkuu wa Azam, Abdilhamid Moallin, kupoteza tangu apewe majukumu hayo mwishoni mwa Januari mwaka huu kwa mkataba wa miaka mitatu.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE SAFI REAL MADRID

KLABU ya Real Madrid bado ina uhakika wa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, kwa uhamisho huru kutoka Paris St-Germain. ***(Goal)***

### MBAPPE MBADALA WA HAALAND

IWAPO klabu hiyo ya Hispania itashindwa kumsajili Kylian Mbappe na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, basi wataelekeza mawazo yao kwa mshambuliaji wa Liverpool mwenye umri wa miaka 29, Sadio Mane. ***(Fichajes)***

### SERGI KUTUA ARSENAL

MATUMAINI ya Arsenal kumsajili mchezaji Sergi Roberto kutoka Barcelona yameongezeka kwani nyota huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 30 bado hajasaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Katalunya. (***Sun***)

### CAVANI KUTUA BOTAFOGO

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 35, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, anasemekana kuwa tayari kusikiliza ofa kutoka kwa klabu ya Botafogo ya Brazil. (***Goal***)

### FELIX ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 22, kutoka kwa mabingwa wa Hispania, Atletico Madrid. (***El Chiringuito, via Mail)***

### NKUNKU KUIGHARIMU UNITED

MCHEZAJI wa RB Leipzig, Christopher Nkunku, ataigharimu Manchester United "angalau euro milioni 75" kama wanataka kumsajili kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. (***Bild***)

### GOMEZ AGOMBEWA ENGLAND

NEWCASTLE na Aston Villa wameongoza mbio za kumnasa Joe Gomez iwapo Liverpool itaamua kumuuza mlinzi huyo wa Uingereza mwenye umri wa miaka 24 msimu huu. (***Athletic***)

### SPURS WAMTAKA DYBALA

KLABU ya Tottenham Hotspur wamejitokeza na "ofa thabiti zaidi" ya kutaka kumsajili mshambuliaji, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28, kutoka Juventus msimu wa majira joto, lakini Barcelona na Inter Milan zinasalia kuwa chaguo la Muargentina huyo. (***Sport***)

### OLISE AWINDWA KILA KONA

KLABU ya Crystal Palace wanakabiliwa na changamoto ya kutaka kumbakisha mshambuliaji wa zamani wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 18, Michael Olise mwenye umri wa miaka 20, ambaye anasakwa na Arsenal, Chelsea na Everton pamoja na Bayern Munich na Lille. (***Sun***)

### MARTINEZ AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanatarajiwa kuanzisha upya nia ya kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 24, ambaye mabingwa hao wa Italia wameripotiwa kueleza kuwa na thamani ya euro milioni 90. (***Calciomercato***)

### JOHNSON KUPEWA MKATABA

KLABU ya Nottingham Forest imeanza mazungumzo ya mkataba mpya na winga wa Wales, Brennan Johnson mwenye umri wa miaka 20 kwa nia ya kuzuia lengo la Brentford, Crystal Palace na West Ham ambazo zinamtaka. ***(Standard)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL ATOA SABABU LUKAKU BENCHI UEFA

**Nilihisi amechoka kidogo na unapaswa kuzingatia kwamba amecheza sana, kwake labda...**

**LONDON,** ENGLAND

THOMAS Tuchel amekiri kwamba, alimweka benchi mshambuliaji, Romelu Lukaku kwa sababu alihisi kiwango duni cha Mbelgiji huyo cha hivi karibuni kimetokana na uchovu.

Lukaku amekuwa mmoja wa wachezaji wanaoanza kikosi cha kwanza cha Chelsea akiwa fiti, licha ya kutofanya vizuri kila mara, lakini uchezaji wake wa kugusa mpira mara saba tu dhidi ya Crystal Palace mwishoni mwa wiki, umemfanya mchezaji huyo aliyeweka rekodi ya usajili wa klabu hiyo kuwekwa benchi katika mechi ya kwanza ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lille, Jumanne.

**"Nilihisi amechoka kidogo. Alionekana amechoka kidogo na unapaswa kuzingatia kwamba amecheza sana," alisema Tuchel kuhusu uamuzi wake wa kumweka benchi.**

"Tumekuwa na muda wa ziada (katika fainali ya Klabu Bingwa Dunia), tukisafiri sana hivi karibuni na haikuwa rahisi kwake dhidi ya Palace, huu haukuwa uchezaji wake bora.

"Kwa hiyo labda itakuwa rahisi kwake kuingia kutokea benchi na kugeuza mambo ikiwa tunamhitaji."

Lukaku alikuwa ameanza mechi kumi za mwisho za Chelsea katika mashindano yote, lakini heshima amepewa Kai Havertz kwa mechi hiyo, huku Mjerumani huyo akianza katika mechi yake ya 50 kwa 'The Blues' hao tangu kuwasili kwake mwaka 2020.

Christian Pulisic naye alianza pamoja na Hakim Ziyech aliyepo kwenye kiwango bora, huku Timo Werner akijiunga na Lukaku kuanzia benchi.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 961,

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
WOLVERHAMPTON
1 | 1.69
X | 3.57
2 | 5.33

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CONTE NA MATUMAINI YA KUMBAKIZA KANE

**LONDON,** England

ANTONIO Conte hana tatizo na "matamanio makubwa" ya Harry Kane na bado anatumaini anaweza kuwa mtu wa kumshawishi mshambuliaji huyo kubaki Tottenham Hotspur.

Kane alishinikiza kuhama Spurs kabla ya msimu huu, huku Manchester City ikionekana kuwa ndio sehemu anayoelekea.

Lakini Tottenham ilisimama kidete na Kane akalazimika kubakia London licha ya yeye mwenyewe kuweka wazi kuwa anataka kuondoka. Nahodha huyo wa England bado anaonyesha nia yake ya kutaka kuihama klabu yake hiyo ya utotoni.

Hata hivyo, mechi ya Jumamosi kati ya Man City na Tottenham ilitoa sababu ya matumaini, huku Kane akiiongoza vema timu yake kushinda mabao 3-2 dhidi ya vinara hao wa ligi.

Kane alifunga mabao mawili na kuchangia moja kwa wageni katika mchezo uliosifiwa sana.

Nia ya Kane ni kushinda mataji inalingana na mipango ya Conte, ambaye ametwaa mataji matano ya ligi katika timu zake tatu za awali Inter Milan, Chelsea na Juventus.

"Harry ni mchezaji mwenye malengo makubwa na lazima iwe hivi, tunazungumza kuhusu mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa," alisema Conte.



## Mourinho afungiwa, apigwa fain

**ROME,** Italia

KOCHA wa Klabu ya AS Roma, Jose Mourinho, amefungiwa michezo miwili na kupigwa faini ya pauni 17,000 baada ya kumshtumu mwamuzi kuwa ametumwa na klabu ya Juventus.

Kocha huyo wa zamani wa klabu za Chelsea, Manchester United, Real Madrid na Inter Milan kwa sasa ana wakati mgumu baada ya kushinda michezo miwili tu kati ya nane ya mwisho kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Kikosi hicho cha Giallorossi kilitoka nyuma na kurudisha mabao mawili na kutoka sare Jumamosi na Verona, lakini "The Special One" huyo alitolewa nje ya uwanja kwa kadi nyekundu.

Mourinho alilimwa kadi hiyo baada ya kukwaru zana na mwamuzi mar kadhaa na kuupiga mpir jukwaani kwa mashabiki.

Chama cha soka nchin Italia kimempiga faini n kumzuia michezo miwil kocha huyo baada ya kum tolea kauli mbaya, mwa muzi Luca Pairetto kuw ametumwa na klabu ya Ju ventus, baada ya kutokuri dhishwa na maamuzi yak kwenye mchezo huo.

HABARI MICHEZO

,840,460

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/02/22 | 18:00 | Brighton vs Aston Villa | 2.32 | 3.25 | 3.10 |
| 02. 26/02/22 | 18:00 | Brentford vs Newcastle | 2.41 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 26/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Hull City | 2.54 | 3.12 | 2.73 |
| 04. 26/02/22 | 18:00 | Millwall vs Sheffield Utd | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 05. 26/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Huddersfield | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 26/02/22 | 19:00 | Sivasspor vs Besiktas | 2.56 | 3.05 | 2.81 |
| 07. 26/02/22 | 20:30 | Oostende vs St Truiden | 2.47 | 3.40 | 2.66 |
| 08. 26/02/22 | 22:45 | Sassuolo vs Fiorentina | 2.75 | 3.44 | 2.47 |
| 09. 27/02/22 | 14:15 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.52 | 3.50 | 2.52 |
| 10. 27/02/22 | 15:30 | Hamburger SV vs Werder Bremen | 2.43 | 3.44 | 2.65 |
| 11. 27/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Konyaspor | 2.45 | 3.16 | 2.86 |
| 12. 27/02/22 | 17:00 | Angers vs Lens | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 13. 27/02/22 | 17:00 | Metz vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 24/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 4961 | BB Erzurumspor U19 vs Bursaspor U19 | 1.92 | 3.57 | 3.33 |
| 13:00 | 5583 | Ararat Yerevan vs Artsakh | 1.92 | 3.18 | 3.80 |
| 14:15 | 2062 | Pusamania Borneo vs Psis Semarang | 1.97 | 3.09 | 3.72 |
| 14:15 | 3674 | Persita Tangerang vs Persepam MU | 2.99 | 3.09 | 2.27 |
| 14:15 | 4289 | Persib Bandung vs Persela Lamongan | 1.23 | 5.22 | 10.64 |
| 15:00 | 2190 | Urartu vs FC Noravank | 1.39 | 4.24 | 6.94 |
| 15:00 | 3101 | KF Gjilani vs KF Dukagjini | 1.21 | 5.57 | 10.57 |
| 15:00 | 5536 | KF Drenica Skenderaj vs FC Prishtina | 2.41 | 2.94 | 2.89 |
| 15:30 | 1814 | Sutjeska vs Jezero | 1.44 | 3.51 | 8.26 |
| 15:30 | 3977 | Decic Tuzi vs Rudar Pljevlja | 1.68 | 3.51 | 4.52 |
| 16:00 | 1149 | Jimma Aba Jifar vs Wolkite City FC | 3.67 | 2.90 | 2.07 |
| 16:45 | 2960 | Bali Utd Pusam vs Persipura Jayapura | 1.31 | 4.53 | 8.67 |
| 16:50 | 2736 | Umm-Salal SC vs AL Wakrah | 2.94 | 3.43 | 2.13 |
| 17:00 | 2639 | Markez Tulkarm vs Tubas | 5.39 | 3.95 | 1.51 |
| 17:00 | 5359 | Delhi Dynamos FC vs ATK Mohun Bagan | 4.06 | 3.86 | 1.68 |
| 17:30 | 4406 | Mornar Bar vs FK Mladost Ljeskopolje | 2.76 | 2.95 | 2.51 |
| 17:30 | 4483 | Petrovac vs Zeta Golubovci | 1.65 | 3.61 | 4.62 |
| 18:00 | 5264 | Queretaro U20 vs Deportivo Toluca U20 | 3.08 | 3.41 | 2.08 |
| 18:30 | 2408 | National Bank vs Pyramids | 4.25 | 2.91 | 2.01 |
| 18:30 | 4737 | Benfica U23 vs Rio Ave U23 | 1.44 | 4.24 | 5.97 |
| 19:00 | 1522 | Al Arabi Doha SC vs Al Khoor | 1.48 | 4.15 | 5.40 |
| 19:00 | 1868 | Al Gharafa SC vs Al Rayyan SC | 2.32 | 3.51 | 2.60 |
| 19:00 | 5131 | Welayta Dicha FC vs Hadiya Hosahina FC | 2.23 | 2.89 | 3.27 |
| 19:30 | 5273 | Iskra vs Buducnost | 2.65 | 3.09 | 2.51 |
| 20:00 | 4454 | Carrarese vs AC Siena | 2.28 | 2.98 | 3.38 |
| 20:15 | 4235 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs AS Tel Aviv University W | 1.93 | 3.72 | 3.19 |
| 20:45 | 1089 | Dinamo Zagreb vs Sevilla FC | 3.40 | 3.40 | 2.12 |
| 20:45 | 1304 | Bodo Glimt vs Celtic | 2.94 | 3.74 | 2.21 |
| 20:45 | 1504 | Partizan vs Sparta Prague | 1.99 | 3.31 | 3.91 |
| 20:45 | 2683 | Karabakh vs Marseille | 3.50 | 3.45 | 2.07 |
| 20:45 | 4569 | Olympiakos vs Atalanta | 3.35 | 3.50 | 2.10 |
| 20:45 | 5005 | Randers vs Leicester | 4.99 | 4.09 | 1.63 |
| 20:45 | 5159 | Real Sociedad vs RB Leipzig | 2.66 | 3.41 | 2.56 |
| 20:45 | 5796 | Maccabi Tel Aviv vs PSV Eindhoven | 3.50 | 3.55 | 2.03 |
| 20:45 | 5940 | Lazio vs Porto | 2.26 | 3.45 | 3.05 |
| 21:00 | 3262 | Pachuca U20 vs Mazatlan FC U20 | 1.75 | 3.61 | 3.95 |
| 21:00 | 3846 | Politehnica Timisoara vs Petrolul Ploiesti | 3.72 | 3.19 | 1.93 |
| 21:30 | 1498 | Spvg Frechen 20 vs Blau-Weiss Friesdorf | 1.35 | 4.98 | 6.32 |
| 21:30 | 2595 | Bangu RJ vs Audax Rio EC RJ | 2.47 | 2.85 | 2.90 |
| 22:00 | 4347 | RS Berkane vs FAR Rabat | 2.26 | 2.80 | 3.33 |
| 22:00 | 5350 | FC Union 60 Bremen vs Leher | 2.32 | 4.05 | 2.36 |
| 22:45 | 2179 | Arsenal vs Wolverhampton | 1.69 | 3.57 | 5.33 |
| 23:00 | 1431 | PAOK vs Midtjylland | 2.07 | 3.24 | 3.74 |
| 23:00 | 1909 | Sporting Braga vs Sheriff Tiraspol | 1.41 | 4.51 | 7.62 |
| 23:00 | 2376 | Vitesse Arnhem vs Rapid Vienna | 1.79 | 3.71 | 4.31 |
| 23:00 | 2455 | Lucchese vs Virtus Entella | 3.08 | 3.13 | 2.35 |
| 23:00 | 4013 | Betis vs Zenit St Petersburg | 2.04 | 3.59 | 3.44 |
| 23:00 | 4318 | Rangers vs Borussia Dortmund | 4.11 | 4.01 | 1.76 |
| 23:00 | 4649 | Slavia Prague vs Fenerbahce | 2.06 | 3.40 | 3.55 |
| 23:00 | 4690 | Napoli vs Barcelona | 2.69 | 3.33 | 2.58 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# SERIKALI, DADA HOOD SASA KUICHANGIA TWIGA STARS

**Na Saada Akida**

SERIKALI kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya 'Dada Hood', inayojishughulisha na kupinga unyanyasaji wa kijinsia, wameandaa tamasha la kuichangia timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake, Twiga Stars.

**Tamasha hilo litakalofanyika Dar es Salaam Machi 8, mwaka huu, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, litahusisha burudani ya muziki na michezo kwa kuchangisha fedha zitakazosaidia kutatua baadhi ya changamoto za timu ya Twiga Stars.**

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha, aliipongeza Dada Hood kwa kazi zao za kuwainua watoto wa kike hasa nia yao ya kuichangia Twiga Stars.

Alisema kujitolea kwa taasisi hiyo iwe mfano kwa Watanzania wengine katika kujitokeza kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kusaidia sekta ya michezo.

"Huu ni mfano wa kuigwa kwa taasisi zingine kujitokeza kuchangia timu za Taifa za Wanawake ili kuendelea kupeperusha bendera ya taifa katika mashindano ya kimataifa," alisema Msitha.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake (TWFA), Somoe Ng'itu, naye aliishukuru serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Dada Hood huku akiwakaribisha wadau wengine kuendelea kuwashika mkono Twiga Stars ili iendelee kupeperusha vema bendera ya nchi kimataifa.

"Dada Hood imefungua milango kwa wadau wengine kujitokeza kusaidia timu za wanawake, maandalizi ya kuandaa timu ni makubwa kwa sababu kuna vitu vingi kama kambi, posho na fedha za usafari," alisema.

Kwa upande wa Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Leah Kihimbi, alisema Rais Samia anaunga mkono kusaidia michezo, hivyo jambo hilo lifungue milango kwa taasisi zingine kuiga mfano wa Dada Hood.

Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Mkuwe Issac 'Mammy Baby', alisema: "Siku hiyo tumeipanga makusudi kwa kazi tatu ambazo ni kufanya harambee kuichangia Twiga Stars, kuzindua albamu ya 'The Orange' na kuonyesha vipaji vya wanawake katika tasnia ya muziki".

# *Geita Gold yaionya Yanga Kombe la FA*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupangwa kucheza dhidi ya Yanga kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, Klabu ya Geita Gold imesema inaandaa mikakati kabambe kuhakikisha inashinda mechi hiyo na kutinga hatua ya nusu fainali.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Felix Minziro, na kinara wa mabao kwenye kikosi hicho George Mpole, wameionya Yanga kuwa isitarajie mteremko, kwani na wao wanahitaji kucheza mechi za kimataifa msimu ujao kwa sababu wana uwezo huo.

"Haikuwa rahisi kutinga robo fainali, lakini tulipambana na sasa tunakwenda kucheza na Yanga, ni timu nzuri na imesajili wachezaji wazuri, ni lazima uwape sifa zao, lakini si kwa sababu ipo vizuri basi tuiogope, hapana.

"Tumeandaa mikakati na tutakwenda kupambana, tutatoa ushindani mkubwa na kuhakikisha na sisi safari hii tunakwenda nusu fainali au fainali kabisa," alisema Minziro.

Naye straika tegemeo kwenye kikosi hicho, anayekamata nafasi ya pili kwa kufunga mabao mengi mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, akiwa amecheka na nyavu mara saba nyuma ya Relliants Lusajo wa Namungo mwenye mabao 10, Mpole amesema wanajua umuhimu wa mashindano hayo, hasa kwenye mechi ya robo fainali dhidi ya Yanga, lakini wamejipanga vema kuikabili.



Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania (TWFA), Somoe Ng'itu, akitoa shukrani kwa BMT na Taasisi ya Dada Hood kwa kitendo cha kuandaa tamasha la kuchangia fedha kusaidia Timu ya Taifa ya Twiga Stars. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Michezo
Alhamisi Februari 24, 2022
Nipashe



Mourinho afungiwa, apigwa faini UKURASA 22

NAPITA!...



Beki wa Kati wa Mtibwa Sugar, Oscar Masai (kulia), akihaha kumdhibiti mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro jana na Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yaweka rekodi

## Kileleni bila kupoteza mzunguko wa kwanza, Mayele apewa ng'ombe...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania, Yanga jana waliweka rekodi ya kumaliza mzunguko wa kwanza bila kupoteza msimu huu, ilipomalizia mechi yake ya 15 kwa kuichapa Mtibwa Sugar mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, mkoani Morogoro.

**Yalikuwa ni mabao mawili ya wachezaji wa kigeni, Mrundi Saido Ntibazonkiza na Mkongomani Fiston Mayele.**

Wakati Ntibazonkiza, anafikisha bao lake la tano msimu huu, Mayele anakuwa na mabao saba, akiwa sawa na George Mpole wa Geita Gold, akimfukuzia kinara wa mabao kwa sasa Reliants Lusajo wa Namungo FC mwenye mabao 10.

Kwa ushindi wa jana, Yanga imeongeza pengo la pointi nane dhidi ya Simba huku timu zote zikiwa zimecheza mechi 15 za mzunguko wa kwanza.

Iliwachukua Mtibwa Sugar dakika 10 za mwanzo kufanya shambulizi langoni mwa Yanga kwa mpira wa kona uliozua kizaazaa, kabla ya kumkuta Mayanja ambaye alipiga shuti lililombabua nahodha Bakari Mwamnyeto, ambalo liliisalimisha timu yake.

Kipa raia wa Mali Djigui Diarra alifanya kazi ya ziada dakika mbili baadaye, alipochupa juu kuokoa krosi ya Salum Kihimbwa, ambayo ilionekana kwenda kutua kwenye kichwa cha George Makang'a.

Hatimaye Yanga ilifanya shambulio la kwanza langoni mwa Mtibwa dakika ya 22, Ntibazonkiza alipounganisha kwa kichwa mpira wa krosi kutoka kwa Djuma Shaabani, huku Mkongomani huyo akiikosesha Yanga bao kwa kupiga shuti kubwa juu ya lango, pale alipotengewa pasi safi kutoka kwa Farid Mussa dakika ya 30.

Yanga iliendelea kukosa mabao, kwani Denis Nkane ambaye alicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kusajiliwa kutoka Biashara United kipindi cha dirisha dogo, alipobaki yeye na kipa Jeremiah Kisubi, lakini shuti lake dhaifu liliishia mikononi.

Nkane, aliyeumia kwenye mechi za Kombe la Mapinduzi na kuwa majeruhi kwa muda, alikosa bao hilo dakika ya 34, akimkabidhi mikononi kipa huyo anayechezea Mtibwa Sugar kwa mkopo, akitokea Simba.

Yanga ilifanikiwa kupata bao dakika ya tano ya nyongeza ya kipindi cha kwanza, baada ya Juma Nyangi kufanya makosa kwa kutaka kupiga chenga na kunyang'anywa papo hapo mpira ukamfikia Feisal Salum aliyempasia Ntibanzonkiza akiwa anatazamana na kipa, akaukwamisha mpira kimyani kulia kwa Kisubi ambaye aliruka upande huo huo bila mafanikio.

Kipindi cha pili, Yanga ilionekana kutoridhika na bao hilo, hivyo kufanya mashambulizi makali langoni mwa wenyeji hasa kupitia upande wa kushoto ambako Omari Sultan alishindwa kabisa kumudu eneo hilo.

Mayele alipachika bao rahisi dakika ya 52, baada ya kazi iliyofanywa na Salum Aboubakar 'Sure Boy', akiwa kwenye winga ya kulia, akamzidi mbio Sultan na kumpasia Ntibazonkiza, ambaye krosi yake ilimkuta mfungaji aliyeusukumizia wavuni. Kwa matokeo hayo Yanga inaongoza kileleni baada ya mechi 15, ikishinda michezo 12, na sare tatu, mabao 25 ya kufunga, ikiruhusu manne, huku Simba ikibaki nafasi ya pili kwa kucheza mechi 15, ikishinda tisa, sare nne na kupoteza miwili, ikifunga mabao 16 na kuruhusu sita.

Mtibwa inabaki kwenye nafasi ya 15, ikiwa na pointi 12, ikizidi Prisons tu inayoshikilia mkia na pointi zake 11.

Baada ya mchezo huo wa jana, shabiki mmoja aliyejitambulisha kuwa ni Mmasai alitangaza kwenda kumkabidhi Mayele zawadi ya Ng'ombe kutokana na kuvutiwa na uchezaji wake.

# Dewji aionya Simba SC CAF

**Na Adam Fungamwango**

MFADHILI wa zamani wa klabu ya Simba, Azim Dewji ameonya timu hiyo kuacha kubweteka na kuridhika pale wanapopata bao moja kwenye michuano ya kimataifa wanayocheza kwani husababisha kushambuliwa na kuruhusu kufungwa kirahisi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Dewji amesema kuwa ameangalia mechi mbili ambazo timu hiyo imecheza na kugundua kuwa ni tatizo kubwa kwenye michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika, kuridhika na bao moja, huku akiipongeza kwa kuongoza kundi mpaka sasa.

"Simba bado wana tatizo kidogo, kwenye ile mechi ya kwanza walipocheza na Asec Mimosas, walipofunga bao moja walionekana kuridhika, wakaanza kupoteza na ilikuwa ni makosa makubwa, kwani baadaye jamaa walirudisha. Baada ya bao kusawazisha ndiyo Simba wakaamka na kuanza kusaka mabao na kweli waliyapata, lakini jambo hili si zuri hata kidogo, wajirekebishe, kama wana uwezo wa kupata mabao zaidi wafanye hivyo kwanza," alisema kiongozi huyo ambaye wakati wa ufadhili wake waliifikisha fainali ya michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka 1993 na kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Stella Abidjan ya Ivory Coastal kwenye Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam, huku tayari ikiwa ilishatoka suluhu ugenini.

Alisema hata timu iliyocheza nayo mechi ya pili US Gendamirie nayo ilipopata bao moja ilianza kujihami na kuipa mwanya Simba kusawazisha bao hilo mwishoni mwa mchezo huo.

"Nao walifanya kama Simba, walijihami wenzao wakarudisha, hii inaonyesha kuwa ni hatari sana kuridhika na bao moja kwenye michuano hii kwa sababu linaweza kurudi muda wote. Cha kufanya kwa Simba ni kwamba kama wana uwezo wa kufunga mabao mawili au matatu wafanye hivyo, halafu baada ya hapo ndiyo wanaweza kuzuia, siyo bao moja," alisema.

Simba ambayo inaongoza Kundi D ikiwa na alama nne, Jumapili wiki hii inatarajia kucheza dhidi ya RS Berkane nchini Morocco kwenye mechi ya kumalizia mzunguko wa kwanza wa michuano hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >